

Huduma ya Uvuvio  
Australia

yawaletea



HATUA  
ZA  
KUUFIKIA

Kuwa hai katika Upako

A small illustration of a campfire at the bottom left. It shows a blue base with orange and yellow flames. Several brown, oval-shaped embers are shown flying out from the fire towards the right, following the curve of the text "Kuwa hai katika Upako".

UVUVIO

## **YALIYOMO**

**Utangulizi: Uvuvio unakuja**

**1a & 1b Kainsa la Siku za Mwisho: Fundisho kutoka Kwa Efeso**

**2. Kuurudia Upendo wa Kwanza: Matendo ya kwanza ni gani?**

**3. Kuumega Mkate katika Maandiko Matakatifu.**

**4. Hakikisho la Wokovu wa Sayuni: Nafasi ya kudumu katika maombi kulingana na Neno la Mungu**

**5. Wokovu kwa Mataifa: Nyumba Yangu itaitwa Nyumba ya Maombi kwa Mataifa Yote.**

**6. Tume Kuu: Mpango wa Uinjilisti.**

**7. Kuingia Katika milango ya Mji Mtakatifu.**

## **UTANGULIZI – UVUVIO UNAKUJA**

Uvuvio ambao unakuja na ambao tayari umeanza katika mataifa mengine ni mavuno katika nyakati za mwisho, ambao ulinenwa mara nyingi na Yesu katika Mafundisho Yake. Sasa Mungu anarejesha huduma ya mitume kwa kanisa na wanaume kwa wanawake walio na maono wameanza kujitekeza katika kazi ya mavuno. Wale ambao wanavazi la utume juu yao wamejitlea kikamilifu kuwafundisha watenda kazi katika mavuno na wengine wameanza shughuli za upanzi wa makanisa.

Katika muongozo huu na katika vipindi ambavyo vitakavyo jitokeza kupitia katika muongozo huu, tutatembelea mafundisho mengine ambayo Bwana ameweka huru.

### **MASWALA BAYANA YA UVUVIO**

1. **Ukweli wa toba** kutokana na dhambi yote na kuungama dhambi kwa Mungu na mtu mwingine kunapohitajika (**Yakobo 5:16**). “*Vivyo hivyo nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu*”, **Rum.6:11**. Mungu analiita kanisa Lake liwetakatifu.
2. **Kuishi na kuenenda kwa Roho, kujifunza kumtegemea Yesu** na Neno Lake kwetu, kupokea na kuitikia upendo Wake, kumtumikia katika maombi na huduma jinsi Anavyoongoza. **Gal.5:16-25**, inazungumzia jinsi ya kuishi maisha ya kushinda mwili kwa kuishi kwa Roho, na kuthihirisha matunda tisa ya Roho. [**Kol.3:1-4**)
3. **Ufupisho wa kazi ya huduma katika maisha ya watu**: jinsi Bwana anvyoifupisha wakati wa huduma kwa kuwaleta watu katika kitu kipyra ambacho Anafanya. Huduma ya ukombozi ni sehemu ya mpangillio huu, pamoja na mwenendo mkuu wa Roho Mtakatifu katika maisha ya watu Wake.
4. **Wajibu Mkuu wa Roho Mtakatifu katika kanisa**, na utiifu usio na swali Kwake katika huduma ya uvuvio. Roho Mtakatifu ni Mungu mionganoni mwetu, **2 Kor. 3:17**, na kupitia kwa ibada ndani Yake tunabadilishwa, **a.18**; na kupitia kwake tunawezeshwa kuwa wahudumu wa Agano Jipyta, **a.5-6**. “Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho hao ndio wana wa Mungu”, **Rum.8:14**.
5. **Kufundisha kutoka kwa Maandiko kuhusu kanisa la kimitume**, kuanzishwa kwake na utekelezaji wa huduma ya kimitume katika kitabu cha Matendo, hasa matendo ya Paulo ya kuanzisha kituo cha mafunzo, ambacho kupitia kwake vuvio nyingi kuu zilikua na kuenea, na watenda kazi wengi waliingia katika kazi ya mavuno. (**Matendo 19:8-10**).
6. **Maombi kama msingi mkuu katika yale Mungu anafanya**: tunakuwa na maombi ya kikundi kila mara na pia tumeongozwa na Bwana katika maombi ya kuugua. Watu wengi hunukuu **Rum 8:28** bila kujua msingi wa **a.26-27** ambao unaonyesha mahali muhimu pa maombi na maombezi ya Roho Mtakatifu kuyaleta mapenzi ya mungu kufanyika.

7. **Kurudia injili na kusikia tena kile Yesu Anasema**, kwa sikio la kusikia kile ambacho analiambia kanisa leo. Ni injili ya Bwana Yesu Kristo(**Marko 1:1**) katika maneno yake amwenyewe. Katika Injili, Yesu anatwambia cha kufanya! Katika kitabu cha Matendo, mitume wanatuonyesha jinsi ya kutii Amri ya Bwana; na katika Nyaraka, mitume wanatwambia kwa nini. Kwa maneno mengine wanafundisha Neno.
8. **Kupenda kuendelea na Mungu kulingana na Neno Lake**, sio kuendelea kufungwa na desturi au utawala. Gharama ni mateso na upinzani!

# **KANISA LA SIKU ZA MWISHO:**

## **FUNDISHO KUTOKA KWA EFESO – SEHEMU A**

### **KANISA LA KIMITUME NI NINI?**

Ni kanisa ambalo Yesu alisema atalijenga katika **Mathayo 16:18**:

"*Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro*

[*Petro ni jiwe, petros; tafsiriwa: Petro, Jiwe*)]

*Na juu ya Mwamba huu {juu ya ufunuo ndani ya Yesu Kristo}*

[*Mwamba = Kristo (S.C.Gr.4073 petra, Mwamba)*

*nitalijenga [Yesu] kanisa Langu wala milango ya kuzimu haitalishinda.*"

Nyumba ya Mungu ya Roho inajengwa na mawe yaliyohai (**1Pet.2:5**). Tunafanyika mawe yaliyohai kwa njia ya imani katika Kristo Yesu!

**Yesu ni mtume**, aliyeleuliwa na Mungu kujenga kanisa, nyumba ya Mungu (**Ebr. 3: 3-6**). Petro kama mtume wa Yesu Kristo, aliteuliwa kuuweka msingi wa kanisa. **Mathayo 16:19**: "*Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga [zuia] duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifunga [ruhusu, haribu]duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.*"

Petro alizitumia hizo funguo Siku ya Pentekoste kuwafungua Wayahudi 3,000 kuingia katika ufalme wa Mungu; alizitumia Samaria kuwafungulia Roho Mtakatifu; na pia alizitumia katika nyumba ya Kornelio kuwafungulia Mataifa wa kwanza kuingia katika Ufalme.

***Kanisa la kimitume*** ni kanisa la Agano Jipy Lake Bwana Yesu Kristo. Hakuna kanisa lingine hakika katika Agano Jipy. Yesu alipatia kanisa mamlaka na uwezo Wake. Aliahidi kuwa "*milango ya Kuzimu*", mamlaka yote na uwezo wa shetani na mapepo wachafu (**Luka 10:19**), hawataweza kushinda kanisa. Ni kanisa ambalo Yesu alituma kuhubiri injili kwa mataifa yote (**Marko 16:15-20 & Mathayo 28:18-20**). Ni kanisa ambalo Yesu aliweka msingi wake katika kuwalea wale mitume kumi na wawili, mashahidi sabini (**Luka 10:1**) na 500 (**1 Kor. 15:6**) waliomuona akiwa hai kutoka kwa wafu. Ni "*Nyumba ya Mungu, ambayo imejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, Kristo Yesu mwenyewe akiwa jiwe kuu la Pembeni, katika yeye jingo lote limeungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana*" (**Efe 2:19-21**).

### **MPANGO WA MUNGU KWA KANISA**

Kitabu cha Efeso kinatupatia picha kamili ya kanisa. Ni Waraka kwa Waefeso ndio Paulo anatoa vipawa vyake Yesu aliyepaa (**Efe. 4:8**). Vipawa ambavyo Yesu aliyepaa alitoa ni: mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu. (**aya 11**). Kristo naye alishuka mpaka pande zilizo chini (mauti, alishuka na akapaa juu – **aya ya 9-10**) ili atoe vipawa na kuwapa watu kwa ajili ya kujenga na kutimiza makusudi ya Mungu. Kanisa la kwanza la Yerusalemu lilianzishwa na wale mitume kumi na wawili na baadaye, liliongozwa na mitume na wazee (**Matendo 15:6**). Muhubiri wa injili, Filipo, (**Matendo 21:8**) kwanza alihubiri Samaria (**Matendo 8:5**) kisha akaacha uvuvio mikononi mwa mtume Petro na Yohana (**aya ya 14**). Kanisa la Antioquia liliongozwa na manabii na waalimu (**Matendo 13:1**), amba mionganoni mwao alikuwa Sauli (Paulo). Ni waraka kwa Waefeso tu ndio unaotuonyesha kazi kamilifu ya kanisa lililofunuliwa na wajibu wake kuelezwawa wazi.

Kitabu cha Waefeso kina mafundisho mengi kuhusu kanisa, ufunuo wa ufasaha amba unaonyesha mpango wa Mungu kwa kanisa. Paulo anasema (**2 Kor. 12:1-4**) alinyakuliwa hadi mbingu ya tatu na akapokea mafunuo, akasikia maneno mengine yasiyotamkika, ambayo

haijuzu mwnadamu ayanene. Je! Kama Musa, aliweza kuonyeshwa mfano wa kanisa la Bwana Yesu Kristo?

## EFESO 1 – SISI NI NANI KATIKA KRISTO

**Aya ya 1:** Paulo anaandika waraka huu kama **mtume** wa Yesu Kristo lakini wengine wanaweza kusema kuwa pia ni nabii kwa ajili ya mafunuo ya Mungu na hivyo inamuweka Paulo kama **mtume na nabii wa msingi** wa kanisa la Bwana Yesu Kristo la Agano Jipy. Anawaandikia **watakatifu** walioko Efeso, wanaomwamini Kristo Yesu. Watakatifu ni waaminio wa kweli wa Mungu, waliotakaswa na Mungu kwa njia ya wokovu Wake.

**Aya ya 2:** Paulo anawatumia salamu za kweli za **NEEMA** na **AMANI** kutoka kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo. Bwana anataka tupokee kutoka kwake neema na amani kila siku. Hii neema na amani ni kweli kila siku – ipokee kwa imani na shukuru Mungu kwa Neema Yake na Amani anayotupatia.

## KANISA LIMEBARIKIWA NA BARAKA ZOTE ZA ROHONI

**Aya ya 3-14:** Paulo anatwambia sote kwa jumla, anaponukuu Baraka nyingi za rohoni ambazo tumepokea kutoka kwake Kristo. Anasema kuwa Mungu ametubariki na kila Baraka za rohoni katika ulimwengu wa roho!

### Baraka hizo ni gani?

1. **Aya ya 4:** *Alituchagua katika Kristo Yesu*
  - a. kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu;
  - b. ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika upendo
2. **Aya ya 5:** Alitangulia kutuchagua ili *tufanywe wanawe* kwa njia ya Kristo Yesu sawasawa na Uradhi wa mapenzi yake;
3. **Aya ya 6:** *Ametuneemisha* katika huyo Mpandwa;
4. **Aya ya 7:** katika Yeye huyo tunao *ukombozi wetu, msamaha wa dhambi*, sawa sawa na wingi wa Neema yake.
5. **Aya ya 8:** *Alituzidishia hiyo neema* katika hekima yote na ujuzi;
6. **Aya ya 9:** Akiisha *kutujulisha* siri ya mapenzi yake, sawa sawa na Uradhi wake alioukusudia katika yeye huyo;
7. **Aya ya 10:** kuleta madaraka ya wakati mkamilifu *atavijumulisha vitu vyote katika Kristo*, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia- katika Yeye huyo.
8. **Aya ya 11:** ndani yake sisi nasi *tulifanywa urithi...*
9. **Aya ya 12:** sisi tuliotangulia kumuwekea Kristo tumaini letu, *tupate kuwa sifa ya utukufu wake*.
10. **Aya ya 13:** *tumetiwa muhuri na Roho Yule wa ahadi aliye Mtakatifu*, tukisha mwamini yeye kwa kulisikia Neno Lake la kweli, habari njema za wokovu wetu;
11. **Aya ya 14:** Roho Mtakatifu ndiye *arabuni ya urithi wetu*, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake (*Rum 8:23*: ukombozi wa miili yetu).

**Kuna baraka 7 kuu ambazo ametoa** kwa ufupi. Hii sehemu ya Maandiko Matakatifu, kuanzia Aya ya 2 ni sehemu muhimu kukaririrwa.

1. **chaguliwa** kabla ya misingi ya ulimwengu;
2. **Tufanywe wanawe;**
3. **Tumekubalika;**
4. ukombozi - tumesamehewa;
5. **tumejulishwa siri;**
6. **Tuna urithi;**
7. **Tumetiwa muhuri** na Roho Mtakatifu.

#### **PAULO ANATUOMBEA: Efeso 1:15-20**

- Aya ya 15** kulingana na **imani yetu** katika Bwana Yesu na **upendo** kwa watakatifu wote;
- Aya ya 16** pamoja na **shukrani** tunatakikana **kuwaombea watakatifu** kwa majina!
- Aya ya 17** Paulo anamuomba **Baba wa utukufu**, Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, atupatie **Roho ya hekima** na ya **ufunuo** katika kumjua yeye [Kristo], na macho ya miyo yetu yatiwe nuru:
- i. mjue **tumaini la Mwito wake.** Linganisha na ombi la Paulo katika **Filipi 3:10-14;**
  - ii. Na **utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu** – Mungu anaurithi wa utukufu ndani yetu, watakatifu wake, “*Kristo ndani yetu!*” (**Kol 1:27**);
- Verse 19:** **na ubora wa ukuu wa uweza wake** ndani yetu tuaminio (kwa sababu tunaamini uweza wa ukuu wake ndani yetu katika Kristo): kwa kadri ya utendaji wa nguvu za uweza wake.
- Urithi huja tu wakati mtu anapoaga. Mungu anatakatufe ili tuweze kuupokea urithi Wake, yaani, Kristo ndani yetu. Tufe ili aishi ndani yetu, utukufu wake ndani yetu na wote wauone. Tunaweza kusema, ‘ukiniona mimi umemuona Yesu?’**
- Aya ya 20** Aliotenda katika Kristo Yesu alipomfufua katika wafu akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho.

**KRISTO YUKO WAPI?** Ameketishwa mkono wa kuume wa Mungu katika ulimwengu wa roho!

- Aya ya 21** **Juu sana kuliko ufalme wote** (utawala) na mamlaka na nguvu (uweza) na usultani, **na kila jina** litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu bali katika ule ujao pia.

#### **Kumbuka, hapa ndipo alipo Yesu!**

- Aya ya 22** Mungu amevitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe **Kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa** (kama kichwa juu ya vitu vyote vya Mungu ambavyo Mungu amepatia kanisa),
- Aya ya 23** Ndilo **Mwili Wake** (sisi ni Mwili Wake)  
(sisi ni) **ukamilifu** wa Kristo anayekamilika kwa vyote katika vyote.  
Kama Mwili wake tunatakikana tumuthihirishe Kristo kikamilifu duniani: Je!  
Twaweza kusema **ukiniona mimi umemuona Yesu?**’

#### **Tunajifunza nini kuhusu kanisa katika sura ya kwanza ya Waefeso?**

- Tumechaguliwa na Kristo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, yaani, kanisa wakati wote limekuwa wazo la milele la Mungu – watu watakatifu wasio na lawama,
- Tumefanya jamii ya Mungu

- Baada ya kukombolewa na kusamehewa
- Na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu.

Mungu hufunulia kanisa kusudi lake la milele, siri, ambayo ni kuvikusanya vitu vyote katika Kristo. Ili kanisa lifahamu kusudi Lake na mpango, Mungu anatupatia Roho wa hekima na ufunuo katika kumfahamu Yesu Kristo na anataka tujulishwe mambo matatu muhimu (*Aya ya 18-20*).

## KANISA LIKO WAPI KATIKA KRISTO?

Kanisa ni Mwili wa Kristo ambaye ameketishwa katika ulimwengu wa roho juu sana kuliko nguvu zote za upinzani. Tunaanza kujifunza kuhusu mahali petu katika Kristo.

### Waefeso Sura ya 2: Mengi kuhusu mahali petu katika Kristo

- Aya ya 1* Tulikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zetu (kwa mwanafunzi anayemaanisha, *Walawi 5:1 - 6:7* inatuonyesha juu ya dhambi ya hatia na sadaka ya kutoa)
- Aya ya 2* ambazo tulizozientea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu na kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi,
- Aya ya 3* ambaao zamani, sisi sote tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na **ya** nia, tukawa kwa tabia yetu ya watoto wa hasira kama na hao wengine.  
(Ni wakristo wangapi bado wanatafuta kutimiza tamaa za mwili na za nia, wakisisisitiza kuwa lazima waelewe mambo yote katika nia zao kabla wahusike, bila kupambanu nia ya Roho?)
- Aya ya 4* Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa **rehema**, kwa **mapenzi** yake makuu aliyotupenda,
- Aya ya 5* hata wakati ule tulipokuwa bado wafu kwa sababu ya makosa yetu; **alituhuisha** pamoja ka Kristo, yaani, tumeokolewa **kwa neema**,
- Aya ya 6* **Akatufufua** pamoja Naye, akatuketisha pamoja Naye katika Ulimwengu wa Roho, katika Kristo Yesu,

## NEEMA YA MUNGU IMEFUNULIWA

- Aya ya 7* ili katika zamani zinazokuja audhihirishe **wingi wa neema yake** upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu. (Mungu atadhihirisha neema Yake kuitia kwetu sisi).
- Aya ya 8* kwa maana mmeokolewa kwa neema, **kwa njia ya imani**; ni kipawa cha Mungu,
- Aya ya 9* wala si kwa matendo.  
Mungu anatonyoshea NEEMA na kutupatia imani ya kuipokea hiyo imani na ndipo tunavyookoka. Neema ni kile ambacho Mungu anatupatia; uweza wake wa kimungu ambayo pasipo hiyo tutahukumiwa. **Neema ni kile Mungu amefanya**; imani ni upande wetu!
- Aya ya 10* sisi tu **kazi ya mikono yake**, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende **matendo mema**, ambayo **tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo**.

REHEMA <i>Aya ya 4</i>	UPENDO <i>Aya ya 4</i>	AMETUHUISHA <i>Aya ya 5</i>	KWA NEEMA <i>Aya ya 5</i>
AKATUFUFUA <i>Aya ya 6</i>	AKATUKETISHA KATIKA KRISTO <i>Aya ya 6</i>		WINGI WA NEEMA YAKE <i>Aya ya 7</i>
KWA NJIA YA IMANI TUMEOKOLEWA <i>Aya ya 8</i>	KAZI YA MIKONO YAKE, MATENDO MEMA YALITENGENEZWA, TUENENDE NAYO <i>Aya ya 10</i>		

**Efe.2:11-13.** Tumeletwa karibu na Mungu kwa nji ya damu yake Kristo; tulikuwa wageni wasio na maagano ya ahadi, tumeferakana na jamii ya israeli = Mataifa katika Mwili, bila tumaini, bila Kristo hamna Mungu duniani.

**Aya ya 14-17** *Yeye ndiye amani yetu*, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mmoja; akibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga, na kuondoa ule uadui kwa mwili wake; ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo;[ambazo hatungeweza kutimiza] ili afanye wale wawili kuwa mtu mpya mmoja ndani ya nafsi yake; akafanya amani kwa njia ya msalaba (tunaweza sote kuja kwa njia ya msalaba; hakuna njia nyingine; kuna mwili mmoja, kwa hivyo kanisa moja). Anakuja kwetu na kutuhubiria amani sisi tuliokuwa mbali, na amani kwa wale waliokuwa karibu. HALLELUYAH!

**Aya ya 18** Kwa maana *kwa yeye* sisi sote **tumepata njia ya kumkaribia** Baba katika Roho mmoja.

#### **WATU WA NYUMBANI MWA MUNGU Efe.2:19-22**

**a.19** “*Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu.*” Watakatifu ni wenyeji wa Yerusalemu ya mbinguni inayoshuka chini duniani kudhihirishwa, na watakatifu ni wenyeji wa nyumbani [nyumba] mwa Mungu.

**a.20** “*Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu Mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni.*” Mitume na manabii ni huduma muhimu ambayo inaweka kanisa kwa msingi sawa sawa juu ya Mwamba amba ni Kristo. Yesu ni jiwe la msingi na tena jiwe kuu la pembeni. Wakati huduma ya mitume na manabii inapokuwa mahali pake basi kujengwa kwa watakatifu ndani ya Yesu Kristo jiwe la pembeni litalainisha – mjengo huu wa kanisa.

**a.21** “*katika yeye jingo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana.*” Kanisa liko linajengwa ulimwenguni kote kuwa hekalu la Mungu.

**a.22** “*Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.*” Kanisa la Mungu ulimwenguni kote lina jumuisha Shirika zote, mahali ambapo watakatifu wanaushuhudia uwepo wa Mungu katika Roho.

# **KANISA LA SIKU ZA MWISHO:**

## **FUNDISHO KUTOKA KWA EFESO – SEHEMU B**

### **EFESO 3: SIRI YA KRISTO NA KANISA LAKE**

- Aya ya 2* Paulo alipokea habari ya uwakili wa neema ya Mungu  
*Aya ya 3-4* kwamba kwa kufunuliwa alijulishwa **siri ya Kristo**;  
*Aya ya 5* Siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi wa Agano Jipyा  
*Aya ya 6* Ni **siri ya Mwili**, unaojumuisha Myahudi na Myunani, kuwa **sisi ni washiriki pamoja na warithi wa ahadi Yake iliyo katika Kristo Yesu kwa njia ya injili.**[kuwa Mungu anawainua waaminio duniani kuwa watu Wake]  
*Aya ya 7* Paulo alikuwa muhudumu wa injili kwa kadri ya kipwa cha neema ya Mungu aliyopewa kwa kadri ya utendaji wa uweza Wake.  
*Aya ya 8* **Hii neema inapatikana** [kwetu pia] kuwahubiri **mataifa utajiri wake Kristo usiopimika**(wasioamini);  
*Aya ya 9* na kuwaangaza wote wajue habari za madaraka[uwakili] ya siri hiyo, ambayo tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu aliyeviumba vitu vyote katika Kristo Yesu;  
*Aya ya 10* ili sasa, **hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi** ijulikane na **falme na mamlaka kwa njia ya kanisa** katika ulimwengu wa Roho,  
*Aya ya 11* kwa kadri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu.

### **Siri ambayo Imefunuliwa Inakabiliana na Upinzani**

*Kuhubiri kristo kunapingwa* katika ulimwengu wa roho **na falme na mamlaka**. Unatafuta kuendelea kumiliki mahali pao kutumia udanganyifu na uoga. Kuhubiri kwa injili [siri iliyofunuliwa] kuna **uweza na mamlaka** kufichua udanganyifu na kuvunja ngome zao zote juu ya nia za wasioamini (*soma funzo hili katika 2 Kor 10:3-6*).

- Aya ya 12* hii ni kwa sababu katika yeye **tunao ujasiri** (wa kukaribia Mungu) katika tumaini kwa njia ya kumuamini Kristo.  
*Aya ya 13* hii injili kuu inafaa kuteseka kwa ajili yake, maana huuleta utukufu kwetu na ndani yetu.

### **OMBI LA PILI LA PAULO KWA AJILI YETU: WAEFESO 3:14-21**

*Aya ya 14* Paulo anampigia magoti Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo (tunafaa kupiga magoti pia).

*Aya ya 15* ambaye kwa Jina lake ubaba wote wa mbinguni na duniani unaitwa (*tumepokea jina jipya, Jina la Mungu wetu*); na sisi ni watu wa jamaa Yake.

*Aya ya 16-19* atujaliaye kwa kadri ya utajiri wa utukufu wake,

1. kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake katika utu wa ndani; (*Matendo 1:8*)
2. Kristo akae miyoni mwetu kwa imani; (*2 Kor 13:5*)
3. tukiwa shina na msingi katika upendo, ili tupate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina – na kujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi;
4. Tupate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu (*Yoh.3:34, Luka 4:18-19*).

**MSTARI WA KUKARIRI:** Efeso 3:20-21 “Basi atukuzwe yeye auezaye kufanya mambo ya ajabu mmo kuliko yote tuombayo au tuyawazayo, kwa kadri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina.”

## Siri

Mungu anafunua siri na kusudi lake na anatupatia uweza wa Roho Wake, imani katika Kristo na upendo wake wa karibu, akitujaza na ukamilifu wake ili kwamba hii siri **ifunuliwe kwa ulimwengu mzima** kuona kwa njia ya Kanisa Lake.

**Yesu Krito ni siri!**

## WAEFESO 4: KUENENDA KATIKA SIRI

### 1. Jamii Ni Moja Na Inatakikana Kukaa Pamoja

- Aya ya 1** kama jamaa ya Mungu, walioitwa Naye, tuenende kulingana na wito tulioitiwa.
- Aya ya 2** kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu tukichukuliana katika upendo;
- Aya ya 3** na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani.
- Aya ya 4** KUNA MWILI MMOJA NA ROHO MMOJA, KAMA MLIVYOITWA KATIKA TUMAINI MOJA LA WITO WETU;
- Aya ya 5** BWANA MMOJA, IMANI MOJA UBATIZO MMOJA;
- Aya ya 6** MUNGU MMOJA, NAYE NI BABA WA WOTE, ALIYE JUU YA YOTE NA KATIKA YOTE NDANI YA YOTE.

### 2. Kuujenga Mwili, Kanisa

**Aya ya 7** kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo. Kila mmoja wetu ana sehemu [kipimo] katika kipawa cha Kristo: **utume, unabii, uinjilist, uchungaji na uwali mu.** Hivi vipawa sio vya watu wachache walichaguliwa ila kwa wote (kila mmoja). Kuna neema maalum ambayo tunapokea kutokana na kila kipawa kwa kila mtu anayepokea huduma hiyo.

Vivyo hivyo, vipawa vya Roho Mtakatifu vinadhihirika kwa kila mmoja wetu (**1 Kor. 12:7**) Mungu amampa kila mmoja wetu kipimo cha imani; (**Rum 12:3**) na katika **Aya ya 6** tumepokea kipawa cha Baba kulingana na neema aliyotupatia kila mtu binafsi.

Vipawa vyote ambavyo vimeandikwa katika Agano Jipyä vinapatikana kwa **kila mmoja na kwa wote**, kwa kadri ya neema na imani. Watu wengi bado hawajafahamu vipawa vya huduma ambavyo Kristo ametupatia. Jinsi Paulo anavyofundisha katika **1 Kor. 12:28** kuna watu ambaa Mungu ameweka kwa ajili ya vipawa Fulani kanisani. Hii inamaanisha kuwa watu wa aina hiyo wana huduma ambayo wanadhirisha kuliko zingine, lakini haimaanishi kuwa wengine hawawezi kuwa na nafasi ya kudhihirisha na kutumika. Pia tafakari kuhusu huduma ya Yesu na ya Paulo. Kunaweza kuwa na kikundi cha utume na cha unabii na kadhalika. Hata hivyo vipawa vyawenza kupita kiasi kuwa mtume anaweza kusafiri na muinjilisti au nabii. Muinjilisti anayefahamika sana William Branham, kila wakati alikuwa akiambatana na mwalimu wa Neno miaka mingi. Alipoanza kufanya mafundisho yeze mwenyewe, akafundisha kimakosa.

**Efeso 4:8:** Kwa hakika Yesu alipeana vipawa hivi wakati alipopaa; ndiposa vinaitwa vipawa vya huduma ya Yesu aliyepaa. Wale wanaopingana kuwa hakuna mitume baada ya mitume wa asili kuaga hawajaelewa mafundisho ya Paulo hapa.

### **3. Vipawa tano vya huduma kanisa limepewa kwa:**

A. kusudi la *kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya huduma itendeke*: je, hiyo kazi ya huduma ni sehemu ya mojawapo wa vipawa tu? Katika msingi wake inaonekana hivyo.

(*kukamilisha Strong's Concordance Greek 2677, inamaanisha kuhitimisha, kuandaa, kufunza, kukamilisha, kukamilisha kwa ajili ya kazi.*)

B. Kufanya kazi ya huduma: kila moja ya wizara tano lazima zifanye kazi katika karama ya huduma ili neema ya Kristo itolewe kikamilifu kwa viungo vyote vya mwili.

C. Hata *Mwili wa Kristo ujengwe*: kulijenga kanisa kuwa kile ambacho Mungu alikusudia kuwa.

(*kujenga fr. S.C. Gr.3619, la maanisha mchoro, mjengo, linatumiwa kumaanisha kujenga; Vines,p.357-8, kujenga nyumba, katika Agano Jipy, kuendeleza kukua kiroho, linatumiwa kwa watu, makanisa, na mwili mzima wa Kristo.*)

### **4. Huduma itakamilika wakati kanisa litakapofikia:**

*Aya ya 13* - *umoja wa imani*  
- *na kumfahamu Mwana wa Mungu,*  
- *hata kuwa mtu mkamilifu,*  
- *hata kufikia kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo.*  
Wakati ambapo watu wameyakubali mafundisho ya watu kuliko ufunuo wa Neno la Mungu lilivyotolewa katika Maandiko Matakatifu (*2 Tim. 3:16-17*) hatutaweza kuufikia ukamilifu huu.

*Aya ya 14* - ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu.  
Kwa sababu ya ukosefu wa wanafunzi wa Biblia ambao ni wanafunzi wa Neno, "*mkiwafundisha kutii yote ambayo Yesu alituamuru sisi*" (*Matt 28:20*), watu wengi hawana msingi imara katika Neno na kwa hivyo wanapeperushwa na kila upepo wa mafundisho ya muhudumu ye yote mwenye ushawishi!

*Aya ya 15* - *Tushike kweli katika upendo,*  
Hili ni gumu kutekeleza kwa sababu ya utoto ndani ya kila mmoja wetu!  
- kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye Kichwa, Kristo

*Aya ya 16* huku kukua ni kwa sababu ya Mwili wote kuungamanika na kushikanishwa pamoja kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga katika upendo. Viungo ni *vikundi vidigo, idara ndogo* ambao hawahudumu tu katika vikundi vyao [ushirika wa kanisa] lakini hufikia mwili mzima. Mwili unajengwa kulingana na kila sehemu ikiwa inafanya kazi. Kisha mwili unakua, ukiwa unajengeka katika upendo kazi inapofanyika.

### **5. Enenda katika utu mpya; Msimhuzunishe Roho Mtakatifu Efeso 4:17-32**

*Aya ya 17* *Msienende kama Mataifa waenendavyo*, katika ubatili wa nia zao,  
Nia ya mwanadadu bila Kristo ni ubatili.

- Aya ya 18** *ambao akili zao zimetiwā giza*, [hadi wamjue Mungu wamo gizani] nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa miyo yao; [tunapomjia Kristo tunarejeshewa mtu wa uzima].
- Aya ya 19** ambaο awali walikufa ganzi wanajitia katika *mambo ya ujisadi wapate kujifanyizia kila namna ya uchafu kwa kutamani*.
- Aya ya 20** Bali ninyi, sivyo mlivyojifunza Kristo:
- Aya ya 21**
- i. *Mlimsikia*,
  - ii. katika yeye *Mlifundishwa*,
  - iii. kama *kweli ilivyo katika Yesu*:
- Aya ya 22** *Mvue* : kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya,
- Aya ya 23** na *mfanywe upya katika Roho* ya nia zenu
- Aya ya 24** mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu, katika *haki na utakatifu wa kweli*. [soma 2Kor.5:17]
- Mpango wa Mungu wa uumbaji ni tuwe kama Yesu.
- Alituchagua ili tufananishwe na mfano wa Mwanawe.
- Aya ya 25** *Uvuenu uongo*, "Mkaseme kweli kila mtu na jirani yake" kwa maana tu viungo, kila mtu kiungo cha mwenzake.
- Aya ya 26** "*mwe na hasira, ila msitende dhambi*"; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka. Kabiliana na kila hasira; sawazisha chanzo chake; mtafute Bwana – ‘Bwana kwa nini nina kasirika haraka?’ kuwa na nidhamu; jua jinsi ya kuwa na kiasi bila kutenda dhambi kwa mdomo wako na matendo yako ya fujo!
- Aya ya 27** *wala msimpe ibilisi nafasi*; tusipotawala hasira yetu, tutampa ibilisi nafasi.
- Aya ya 28** *usiibe tena*, bali afadhali ufanye juhudī ukitenda kazi hiyo nzuri kwa mikono yako mwenyewe, upate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. Amini Mungu kwa ajili ya Kazi! Anza kuwasaidi wengine.
- Aya ya 29** Bwana anahaja ya kutakasa kila Neno litokalo katika vinywa vyetu: je, mazungumzo yetu yanajenga na kuwapa neema wanaosikia?
- Aya ya 30** *Wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu!* Dhambi inamhuzunisha Roho Mtakatifu.

<b>Aya ya 31-32</b>	<b><u>Uvueni</u></b>	<b><u>Uvaeni</u></b>
	<b>uchungu</b>	<b>iweni wafadhili</b>
	<b>ghadhabu</b>	<b>wenye huruma</b>
	<b>hasira na kelele</b>	<b>mkasameheane</b>
	<b>matukano</b>	<b>ninyi kwa ninyi</b> ,
	<b>ubaya</b>	<b>kama na Mungu alivyo wasamehe ninyi</b>

## WAEFESO 5: ENENDA

**Aya ya 1** “*Mfuateni mungu kama watoto wanaopendwa*”.

**Aya ya 2-7** **MKAENENDE KATIKA UPENDO**, kama Kristo alivyoenenda akonyesha mfano, kujitolea mwenyewe, achana na kila aina ya dhambi ya mwili. Kinyume cha kuenenda katika upendo ni kuenenda katika mwili; dhambi za mwili hutokana na ubunafsi na kujipenda.

**Aya ya 8-14** **MKAENENDE KATIKA NURU**, dhihirisha tunda la Roho, msiwe na ushirika na giza tena. Kinyume cha kuenenda katika nuru ni kujihuzisha na kila namna ya uchawi na mafundisho ya mashetani, “*matendo yasiyozaa ya giza*”.

**Aya ya 15-21 MKAENENDA KATIKA HEKIMA**, mfahamu ni nini mapenzi ya Bwana, mkijazwa na Roho Mtakatifu, mkinyenyewekeana. Kinyume cha kuenenda katika hekima ni “*kulewa kwa mvinyo*”, ambamo mna ufisadi.

### **Efeso 5:22-33: Siri Ya Kristo Na Kanisa**

Mfano wa ndoa:

1. Kristo ni **Kichwa** cha kanisa.
2. Kristo ni **Mwokozi** wa Mwili.
3. **Kanisa limitii** Kristo katika kila kitu [kanisa liko chini ya Kristo].
4. Kristo **alilipenda kanisa** na akajitolea kwa ajili yake.
5. Kristo **analitakasa na kulisafisha** (kulitenga) kanisa kwa maji katika Neno.
6. Kristo **anajiletea** kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa.
7. Bwana analipenda kanisa; **Anaulisha na kuutunza**.
8. sisi ni **viungo vya Mwili Wake**, wa nyama Yake na mifupa Yake; linganisha **Mwanzo 2:23**.

**Aya ya 31 imenukuwa kutoka Mwanzo 2:24**

**Aya ya 32** Siri hiyo ni kubwa! Bwana anatuita **tutoke katika ‘makanisa ya watu’** tufanyike Bibi arusi wake. Bwana anatamani kufunua na kudhihirisha upendo Wake Mkuu kwetu binafsi na kanisa kwa jumla. Tunapofunguliwa katika Upendo Wake, ataweza kutufikia kwa rahisi na kutakuwa na uhusiano wa mtiririko, tukitimiza makusudi Yake na mipango Yake.

### **TAMATI**

**Sura ya 6** inazungumzia kwa ufupi juu ya **uhusianno wa mzazi na mtoto** na kwa ufupi kuhusu wafanyakazi (watumwa) na bwana wao. Kisha **Aya ya 10-19** zinajulikana vema katika Maandiko Matakatifu juu ya silaha za Mungu (ambazo tunafundisha katika muongozo wa "Uweza wa Maombi").

**Tambua kuwa mafundisho juu ya silaha za Mungu na vita vya rohoni dhidi ya nguvu za uovu zinakuja baada ya Sura tano za kanuni juu ya kanuni na amri juu ya amri ya:**

1. sisi ni nani katika Kristo,
2. kuishi katika (au vaeni) utu mpya,
3. nafasi na urithi wa kanisa,
4. siri ya kanisa inafunuliwa,
5. huduma kamilifu ambayo inaleta kanisa katika ukamilifu (utimilifu),
6. na ufunuo wakanisa ambalo ni Bibi-arusi.

Hili ndilo kanisa! Hawa ni watu ambao wamejiweka tayari kupigana vita dhidi ya adui na kupigia mbiu Neno la Mungu.

Salamu za mwisho za Paulo zinadhihirisha haja ya mawasiliano huru kwa kuituma barua na ndugu mwaminifu kushiriki na watakatifu wa Efeso. Anawaamkua kwa amani na upendo pamoja na imani kutoka kwa Mungu Baba na Bwana wetu Yesu Kristo. Paulo anaonyesha uhusiano wa karibu na Mungu Baba na Yesu ambao unapatikana na wa kweli kwa wale wanaompenda Bwana Yesu Kristo katika hali ya kutokuharibika. Amina.

## **KUURUDIA UPENDO WA KWANZA:**

### **KUFANYA MATENDO YA KWANZA**

#### **Ufunuo 2:4-5**

Hii nisehemu wa waraka ambao Yesu aliandikia kanisa la Efeso. Historia inatwambia kuwa kanisa hili lilikuwa na nguvu sana.

Yohana alimuona Yesu katikati ya *vinara saba vya dhahabu* (*Ufu.1:13*). Vinara saba vinawakilisha makanisa saba (*Ufu. 1:20*).

Katika *Aya ya 2 na 3* Yesu analisifu kanisa maana halikudanganyika na manabii wa uongo na hawakuchoka katika kumtumikia Bwana. Funzo kwetu ni kuwa tutachoka tu wakati tunafanya mambo kwa nguvu zetu. Tukiwa tunafanya kazi ya Mungu, anatutia mafuta kwa ajili ya hiyo kazi.

Katika *Aya ya 6* pia wanasiwi kwa sababu ya kuyachukia metendo ya Wanikolai (ni wale wanaowashinda watu). Hili linazungumzia juu ya mgawanyiko kati ya makuhani na wakristo wa kawaida na imani na matendo ambapo ukuhani unapewa afisi Fulani za juu na huduma za kutekeleza na wanafundishwa kufanya hivyo, kwa kuwafanya watu wahudumu tu katika mazingira madogo ya huduma, badala ya kuwajenga na kuwatuma katika huduma na kuwakuza watu wa Mungu.

*Aya ya 7* ni ahadi “*yeye ashindaye nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu*”. Hii ni ahadi ya sasa. Yesu anasema kuwa ikiwa utaenenda katika yale Nisemayo, haya ndio utakayoona.

*Aya ya 4 na 5*: “*Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wa kwanza. Basi kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukafanye matendo ya kwanza. Lakini usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu*”

Kuna mambo manne muhimu katika aya hizo:

1. ***Umeuacha upendo wa Kwanza*** – tunatakitana kutambua kuwa tumeuacha upendo wa kwanza.
2. ***Kumbuka ni wapi ulikoanguka*** – tumeanguka kutoka mahali Fulani, panapoitwa upendo wetu wa kwanza. Anguko la kwanza lilikuwa kule Edeni na Adamu na Hawa wakaondolewa bustanini. Kuurudia upendo wa kwanza kunatupatia nafasi ya kurudi kwenye mti wa uzima, ambako kuna furaha ya kuweza kutembea na Mungu tena na kuisikia sauti Yake, katika Paradiso.
3. ***Ukatubu na kufanya metendo ya Kwanza***. Kutubu ni kubadilika, **geuka kutoka kwa yale umekuwa ukifanya**. Usipotubu, Yesu atakuja na kukiondoa kinara cha taa kutoka mahali pake.
4. ***Yesu anatishia kukiondoa kinara cha taa mahali pake*.**

## KINARA CHA TAA NI NINI?

1. Kinara cha taa kinaangaza – *Yesu ni Nuru. Yoh. 1:4-5:* “Ndani yake ndimoulimokuwa uzima, na ule uzima ulikuwa nuru ya watu, nayo nuru yang’aa gizani, wala giza halikuishinda.”

*John 8:12:* Yesu akawambia, “Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.”

**Yesu anasema: “Nitaondoa Uwepo Wangu!”**

2. Nuru inatoka kwa mafuta yanayochomeka, kwa kuwasha utambi ambaa unaingia kwenye mafuta. Mafuta yanayochomeka yanawakilisha *Roho Mtakatifu ambaye anatia nuru katika ufahamu wetu. Efeso 1:18-19:* Roho Mtakatifu anatia nuru ili “... macho ya miyo yenu yatiwe nuru kujua;

a. *Tumaini la mwito wake*

b. *Na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo, na*

c. *Na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo kwa kadri ya utendaji wa nguvu za uweza wake*.

Roho Mtakatifu anaondoa utaji kutoka mioyoni mwetu ili tuweze kuyaelewa Maandiko Matakatifu.

*2 Kor. 3: 15-16:* mtu anapomrudia Bwana utaji unaondolewa.

*2 Kor. 4:6* Bwana ameangaza nuru yake Miayoni mwetu na kufunua yale tunayostahili kujua kuhusu Mungu ambayo Kristo amedhihirisha.

**Yesu akiondoa uwepo wake, Roho Mtakatifu hatakuwepo pia.**

3. Kinara cha taa, kilichojaa mafuta, *kinazungumzia watakatifu* wanaojiandaa kukutana na Bwana Arudipo.

*Matt. 25:1-13:* katika mfano wa wanawali wenye busara walikuwa na mafuta mengi; walikuwa wamejiandaa kwa kurudi kwake Bwana. Wale wapumbavu hawakuwa tayari; hawakuwa na mafuta ya kutosha kuwasha taa zao.

*Wanawali wapumbavu waliupoteza uwepo wake.*

4. Kinara cha taa kinawakilisha *kanisa katika roho. Ufu. 1:20* “vinara vile saba ni makanisa saba.” *Ufu. 1:13* inatwambia kuwa Yesu yuko katikati ya vinara. Yeye ameketi kwenye Kiti cha Enzi katika kanisa Lake. Ni kwa njia ya kanisa Yesu anatawala duniani na ulimwengu wa roho, akivijumulisha vitu vya mbinguni na duniani. Yesu akiondoa kinara cha taa, ‘kanisa’ linalobaki sio kanisa Lake tena! **Nuru na uhai vimeondoka!**

**Kutajwa mara ya kwanza kwa kinara cha taa ni katika Kutoka 25:31-40** ambapo Mungu anampa Musa maagizo kuhusu ujenzi wa Hema.

1. Ilitengenezwa na *dhahabu safi*. Hii inazungumzia utakatifu. Wasafi wa moyo watamuona Mungu (*Matt. 5:8*). Imani safi inamdhahirisha Mungu. **[Kutoka 25:31]**

2. Kilitengenezwa kwa kazi ya kufua. Kusudi la Mungu ni kuwako kwa *kanisa moja*, mfano wa mtu asafishaye fedha kwa moto, kulingana na Neno la Mungu lililo safi. **[Kut.25:31]**

3. Kilirembeshwa kwa maua ya mlozi. Maua ya mlozi ni ukumbusho wa fimbo ya Haruni iliyochipuka, (*Hes.17:1-10*) tawi kavu lililofanywa uhai tena, likiwakilisha *upako, maisha ya ufufuo*. {pia *Yer.1:11-12*} **[Kut.25:33-34]**

4. Kinara cha Taa kilikuwa na vikombe vya kushikilia mafuta, upako unastahili kukaa ndani yetu. **[Kut.25:33] 1 Yoh. 2:20, 1 Yoh. 2:27**

5. **[Kut.25:37]** Kinara cha Taa kinaangaza. Nuru ya Kristo iko kanisani, ndiyo nuru inayoangaza dunia. *Isaya 60: 1-3:* “Ondoka uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja.”

6. Kinara cha Taa kilitakikana kutengenezwa kulingana na maono ya mbinguni. Mungu analiandaa kanisa Lake kulingana na maono ya mbinguni. *Efe.3:8-12* “Kwa kadri ya kusudi la milele alilokusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu.”*a.11*)

Tunaishi katika siku za urejesho. Kanisa bado halijaumbika katika mfano wa mbinguni. Kurudia upendo wa kwanza na kufanya matendo ya kwanza ni hatua ambazo kanisa linatakiwa kuchukuwa kutimiza mfano wa mbunguni.

Kanisa bila kinara cha taa ni kanisa lenye mfano wa utauwa lakini linakana nguvu zake (*2 Tim. 3:5*).

Kanisa litawezaje kukaa bila upendo wa Kristo? Tubu haraka! Rudia matendo ya kwanza, ondoka katika ukosefu wa upendo na utende yapasayo.

### **MATENDO YA KWANZA NI GANI?**

- (a) Yale *yanayodhahirisha upendo wa kwanza* ambao Yesu anahitaji.  
(b) Upendo wa kwanza si hisia zile ulizokuwa nazo wakati ulipookoka.  
(c) Upendo huu ni *Agape* katika Kiyunani. Ni upendo wa kujitolea, sio wa hisia.

Maana ya upendo wa kwanza ni:- hamu nzito ya kumtumikia Bwana, kwa kumwambia kila mtu juu ya wokovu, kusoma Neno na kuomba. *Upendo wa kwanza ni sawa na matendo ya kwanza.*

**Kanisa la kwanza lilifanya nini kilicho mpendeza BWANA?** Kanisa la kwanza lilizaliwa Siku ya Pentekoste. *Matendo 2:42* yatufunulia matendo ya kwanza. Kanisa la kwanza lilidumu katika mambo manne;

1. Fundisho la mitume;
2. ushirika;
3. kuumega mkate;
4. kusali.

#### **1. Fundisho la mitume**

Hili ni Neno safi la Mungu. Yesu aliwaamuru wanafunzi wake kufundisha Neno. *Matt. 28:20*: “... *mkiwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi.*” Mafundisho ya Neno ni muhimu kwa uhai wa kanisa. Watu wa Mungu mara nyingi wamefundishwa Neno la Mungu. Mtume Paulo alifundisha Neno la Mungu kila sikua (*Matendo 19:9-10*), na nyumba kwa nyumba (*Matendo 20:20*). Ni wazi kuwa tendo la kwanza ni kufunza neno. Kila mkristo anatakikana kuwa mwanafunzi wa Neno la Mungu. Tunatakitana kulijua Neno la Mungu ilituweze kulifunza!

#### **2. Ushirika**

kiyunani: kushirikiana, umoja, uhusiano wa karibu, kuhusika, jumuia, Meza, ushirika, Chakula cha Bwana, mchango, undugu. ‘*Koinonia*’ ni umoja ambao unaletwa na Roho Mtakatifu. Katika ‘*Koinonia*’ mtu anashiriki vitu vyake vyaya kawaida katika ushirika wa karibu pamoja na jumuia ya wakristo. ‘*Koinonia*’ unajenga uhusiano wa Mkristo na Bwana Yesu na kati ya mmoja na mwengine. Ushirika unaleta *Matendo 2:44-45*: “*Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika wakiuzamali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja.*”

#### **3. Kuumega mkate**

Kuna wakati ambapo kumega mkate ni sehamu ya Chakula cha Bwana kabla na baada ya kufufuka kwa Yesu: *Matt. 14:19*, kuwalisha wale elfu tano; *Luka 24:30*, Yesu

alipoumega mkate na wanafunzi njiani Emau; **Matendo 20:7 na 11**, kuumega mkate ulikuwa sehemu ya chakula.

Katika **1 Kor. 10:16** Paulo anaelezea kuwa kumega mkate ni kama kula mwili wa Kristo. Kwa hivyo inaoonekana kuwa kufikia hapo kuumega mkate ultambulika kuwa sehemu ya Chakula cha Bwana. Paulo pia anatoa maagizo kuihusu katika **1 Kor. 11:23-26**. Tunatakitana kuja mezani pa Bwana kila

wakati tukimkumbuka Yesu. Kanisa la kwanza liliomega mkate kila siku (**Matendo 2:46**).

#### 4. **Kusali**

Maombi ya kikundi. Mikutano ya maombi ya wazi - Matendo 3:1: katika mjengo wa kanisa (hekaluni); Matendo 16:13: hadharani.

Kanisa linahitajika kukutana wakati wote na kuomba; tendo la kuhusika, muhimu kwa uhai wa kanisa. Watu wanakutana pamoja kuutafuta uso wa Bwana, kusikia kutoka kwa Mungu na kuomba mapenzi ya Mungu.

Maombi ya aina hii yata;

- Leta mwangaza wa Yesu katika hali;
- Leta upako;
- Leta ufunuo wa Neno la Mungu;
- Leta wokovu wa waliopotea.

Kuna mikutano mikuu ya maombi ambayo imenukuliwa katika kitabu cha Matendo ya Mitume.

**Matendo 4:23-31:** matokeo ya mikutano ni kuja kwa Roho Mtakatifu na wakahubiri Neno la Mungu kwa ujasiri.

**Matendo 12:5:** Maombi yalifanywa kwa niaba ya Petro alipokuwa gerezani; hii ilifanya aachiliwe kutoka gerezani.

**Matendo 12:12:** wengi walikusanyika katika maombi

**Matendo 13: 1&3:** Roho Mtakatifu alikuwa akiongoza mikutano hii ya maombi, matokeo ni kutawazwa kwa mitume wengine.

Katika **1 Tim. 2:1-2** tunaambiwa kuwa sala, dua, maombezi na shukrani ifanywe kwa ajili ya watu wote, pia kwa wafalme na wote waliko kwenye mamlaka. **Aya ya 8:** “*Basi nataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyo takata pasipo hasira wala majadiliano.*”

#### **Kuna matarajio gani wakati kanisa linaporudia upendo wa kwanza na kutenda matendo ya kwanza?**

Kujitolea katika matendo ya kwanza kuliashiria jumuia mpya. Uwepo wa Mungu ulidhihirika mionganini mwao, (a.43) ishara na ajabu nyingi; (a.44-45) kiwango cha ushirika na kushirikiana hadi waliokuwa nje wakashaaanga na kusema, “*jinsi wanavyopendana*”. Hii jamii ilikuwa wakati wote pamoja na kumega mkate ulikuwa jambo kuu katika ushirika wao na Bwana Yesu.

**Matendo 2:47:** matokeo ni watu wa sifa ambao wamewapendeza watu wote. Hili ni kanisa ambalo Mungu aliongeza kila siku wale waliokuwa wakiokoka. Timazi ambayo tunapimwa nayo tunapourudia upendo wa kwanza ni: je, watu wanaokoka? **Matokeo yanatakitana kuleta wokovu wa nasfi nyingi.**

# **KUUMEGA MKATE KATIKA**

## **MAANDIKO MATAKATIFU**

Kulingana na **Matendo 2:42** kanisa la kwanza lilidumu katika mambo manne:  
**Fundisho la mitume, Ushirika, Kuumega mkate na Kusali.**

Katika kipindi hiki, tunaangalia yale Maandiko Matakatifu yanayosema kuhusu **kuumega mkate**. Kuumega mkate ni kufanya yale Yesu alifanya usiku ule amba alitolewa, “*Alitwaa mkate, naye akiisha shukuru akaumega, akasema huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu*” (1Kor.11:23-24). Haizungumzii kula chakula pamoja tu. Hii ni wazi kutoka kwa Matendo 2:46 ambapo mkate unatajwa pamoja na kula chakula, na katika Matendo 2:42 inaandika kumega mkate kama tendo la muhimu katika mambo yale ya kanisa la kwanza. Hakuna jambo la ajabu wakati wakristo wanaposhiriki chakula nyumbani, lakini kuna kitu cha nguvu, cha Kimaandiko na ambacho kinamuweka Kristo katikati yetu tunapomega mkate pamoja kwa kumkumbuka Yesu.

**1 Kor 10:16:** “*Kikombe kile cha Baraka tukibarikicho, je! Si ushirika wa damu ya Kristo? Na mkate ule tumegao, si ushirika wa mwili wa Kristo?*”

**Neno meza hapa ni la Kiyunani “Koinonia”**  
**Kumaanisha ushirika ama kushirikiana.**

Wakati ambapo tunaumega mkate na kikombe, tunakuwa na ushirika pamoja na ama tunashirikiana katika mwili na damu ya Yesu Kristo. **1 Kor. 11:24:** Yesu alisema kuwa mkate tuumegao ni mwili Wake uliovunjwa kwa ajili yetu. Alisema, “*fanyeni hivi kwa kunikumbuka.*”

**Aya ya 25:** “*Kikombe ni kikombe cha Agano Jipyä*”; damu aliyomwaga kwa ajili yetu.

**Aya ya 26:** kila wakati tunapoishiriki meza ya Bwana tunatangaza mauti ya Bwana hata ajapo.

Tunakumbuka kifo cha Yesu na tunatazamia kurudi Kwake. Tunatambua sadaka yake kwa ajili ya dhambi zetu na kuititia kwa kujitolea kwake tunapokea msamaha Wake na kutakaswa maishani mwetu. Tunapokea kutoka kwa ufufuo wake na kupaa kwa nguvu na kulitimiza Neno Lake katika kizazi hiki.

### **MEZA YA KWANZA**

**Meza ya kwanza** katika Biblia imeandikwa katika **Mwa. 14:18-20.** Abramu akirudi kutoka kwenye vita ambapo alimshinda mfalme wa Sodoma; alikutana na Melkizedeki. Melkizedeki akamtolea mkate na divai. Yeye alikuwa Mfalme wa Salemu na kuhani wa Mungu aliye juu sana. Alimbariki Abramu na kumwambia, “*ubarikiwe Abramu wa Mungu Aliye Juu Sana, muumba mbingu na nchi; Ahimidiwe Mungu Uliye Juu Sana, aliyewatia adui zako mikononi mwako.*” Abramu akampa fungu la kumi la vitu vyote.

Melkizedeki pia anatajwa katika **Ebr. 7:1-3.** Tumeambiwa kuwa jina lake linamaanisha “*mfalme wa haki na mfalme wa amani*”. Hana baba wala mama, hana wazazi, lakini ana mfano wa Mwana wa Mungu na anabaki kuwa kuhani milele. Mfalme na kuhani anahudumia mtu wa imani mkate na divai! Ibrahim, mtu wa imani, alipokea **mkate na divai** kutoka kwa Mfalme wa haki, mfalme wa amani, ambaye ni kuhani wa Mungu Aliye juu sana.

## DAMU YA AGANO NA CHAKULA KINGINE MAALUM

Katika **Kutoka 24** chakula kingine maalum kimenekuliwa. Israeli walikubali kwa sauti moja kuhusu Agano ambalo Mungu alifanya pamoja nao na kusema, “**Maneno yote aliyoyanena BWANA tutayatenda.**” (a,3).

Musa akaitwaa damu na kunyunyiza nusu yake kwenye madhabahu na nusu nyininge kwa watu akisema, (*Aya ya 8*) “**Hii ndiyo damu ya agano alilolifanya BWANA pamoja nanyi katika maneno haya yote.**”

Kisha *Aya ya 9-11* Musa, Haruni, Nadabu na Abihu na watu sabini mionganoni mwa wazee wa Israeli wakakwea juu mlimani wakamuona Mungu wa Israeli. Walikuwa wamefunkwa tu na damu na kwa hivyo **kitambaa kilikuwa kimeinuliwa** wakawezeshwa kumuona Mungu na Maandiko yanasema **wakala na kunywa**. Hatuambiwi ni kitu gani walikula lakini tunajua walikuwa wakihusika katika chakula maalum pamoja na BWANA mwenywewe.

## MAFUNDISHO KUHUSU SADAKA ZA KILA SIKU

### KUTOKA 29:38-46

*Aya ya 38 na 39* Wana Kondoo wawili walichinjwa kila siku kama sadaka, mmoja asubuhi na mwengine jioni. Sehemu muhimu ya sadaka ya kila siku alikuwa ni Mwana kondoo.

*Aya ya 40:* Asubuhi waliongeza kwa hiyo sadaka unga mzuri, na mafuta na divai.

*Aya ya 41:* Jioni waliongeza **unga na divai pekee yake.**

Mafuta yanawakilisha upako wa Roho Mtakatifu. Ni jambo la muhimu tunapokuja mezani pa Bwana na kuupokea upako wa uponyaji, Baraka, wa uhuru, na wa huduma.

**Yesu amefanyika Mwana Kondoo wa sadaka, kwa hivyo hatuhitaji kutoa sadaka ya mwana kondoo, bali amatuacha na unga [mkate] na divai.**

*Aya ya 42:* Sadaka ilifanyika mlangoni pa ile hemu ya kukutania mbele ya BWANA na BWANA anasema hapo ndipo mahali tutakapokutania nanyi. Tunapokutana na kushirikiana naye katika kuleta sadaka ya kila siku, atalitimiza Neno Lake la kukutana nasi na kunena nasi.

*Aya ya 43:* Wakati Mungu anaposhuka na kukutana na watu Wake, utukufu Wake upo mahali pale. Mungu atamimina utukufu Wake juu ya watu Wake.

*Aya ya 44-46:* Mungu anaahidi kuwa atakaa na wana wa Israeli na kuwa Mungu wao.

## Ni kwa msingi gani Mungu atakaa katika Kanisa Lake na kusema sisi ni watu Wake?

Ni kwa sababu tunahusika katika **sadaka ya kila siku ya Mwili na damu ya Yesu kama Mwana Kondoo wa sadaka** unaoleta wokovu. Inaonyesha kuwa tumetoka ulimwenguni na tunajitenga kwa ajili ya Mungu. Tunaoshwa na utukufu Wake tunavyokutana naye kila siku na kushirikiana naye. Tunatakikana kuja kwake kila ashubuhi na jioni tukitambua kile ambacho ametufanyia na kutoa shukrani kwa ajili ya wokovu wetu. Makanisa mengi hayajasherehekeea Meza ya Bwana mara kwa mara, na sadaka ya kila siku ilifanywa mara mbili kwa siku. Kutoka kwa mfano huu, tunaona kuwa Meza ya Bwana inatakikana kusherehekewa mara kwa mara, hata kila siku!

Wakati watakatifu watakapurudia mitindo wa kuumega mkate kila wakati na kumkumbuka Yesu jinsi alivyotuamuru, tutaushuhudia uwepo wake mionganoni mwetu kwa njia kuu, na watu wataokolewa. **Yohana 12:32-33**, “**Nami nikiinuliwa juu ja nchi, nitawavuta wote kwangu. Aliyanene hayo akionyesha ni mauti gani atakayokufa**” Katika kuumega mkate, tunakuwa tunamuhubiri Yesu alivyo na kwa nini alikufa msalabani.

## PASAKA

**Kutoka 12:1-28** inanukuu Pasaka ya kwanza. Mwana Kondoo alikuwa kiungo cha muhimu cha sadaka. Alihitajika kuwa bila mawaa. Watu waliila nyama na kupaka damu kwenye kizingiti cha juu ya mlango na katika miimo miwili ya nyumba zao. Kumwagwa kwa damu

kuliwakinga dhidi ya kifo wakati ambapo malaika wa kifo alipopita juu ya nchi. Waliila nyama ya Mwana Kondoo na kuondoka Misri. ***Mwili [nyama] ya mwana Kondoo iliwahifadhi safarini wakitoka Misri na damu iliwakinga kutoka kwa adui au mharibifu!***

Ulikuwa wakati wa chakula cha Pasaka ya kila mwaka ndipo Yesu alianzisha Meza ya Bwana. Yesu alipokufa msalabani, aliimwaga damu Yake na hiyo damu Yake inatufunika.

***“Huu ni Mwili wangu uliofunjwa kwa ajili yenu. Hii ni damu ya Agano Jipyia aliyomwaga kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu.”***  
**(Matt. 26:26 na 28)**

***Yohana 1:29: “Tazameni Mwana Kondoo wa Mungu achukuaye dhambi za dunia.”***

Yesu ni Mwana Kondoo wa Mungu achukuaye dhambi; ***Yeye ni Pasaka Yetu!***

Katika meza tunautwaa mkate na kula tukimkumbuka Yesu, nakuupokea uponyaji **“kwa mapigo Yake”** (1Pet.2:24); Mwana Kondoo aliyechinjwa kwa ajili yetu; na tunashiriki kikombe, kuwakilisha damu yake iliyomwagiga kwa ajili ya dhambi zetu.

## **MEZA YA MKATE WA WONYESHO**

Moja wapo wa vyombo vitatu katika Mahali Patakatifu katika hema ya Musa ni Meza ya mkate wa Wonyesho. Juu yake kulikuwa na mikate kumi na miwili na **“vyungu na makopo yake”** **Kutoka.25:29.** Kulikuwa na mkate pamoja na divai mezani: **mkate na divai pamoja** katika Mahali Patakatifu, kuelekezea Meza ya Agano Jipyia ilioanzishwa na Bwana Wetu Yesu Kristo.

## **KANISA LA KWANZA LILIMEGA MKATE KILA SIKU**

**Matendo 2:46** **“na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba.”** Kanisa la kwanza walimega mkate kila siku kama sehemu ya ya ushirika. Bwana anarejesha kumega mkate na kikombe kwa kanisa Lake.

Kulingana na Maandiko hakuna sheria ya **mara ngapi** tunastahili kushiriki meza. Lengo ni Yesu; tumkumbuke tunaposhiriki pamoja naye. Kumega mkate kunaweza kufanywa nyumbani na mahali popote ambapo kuna wawili ama watatu wako pamoja katika jina Lake (**Matt.18:20**). Makanisa mengine yameongeza sheria nyingi katika kumega mkate; ni wakati wa kurudia meza kulingana na Maandiko. Hii ni muhimu kwa uvuvio na urejesho.

**1 Kor. 11:28** Tujihoji sisi wenyewe kabla ya kushiriki mkate na kikombe kwa sababu alaye na kunywa kikombe kwa njia isiyofaa anajiletea hukumu.

**Aya ya 30** inasema kwa sababu hii wengine wamekuwa wanyonge na wagonjwa mionganoni mwenu na wengine wamelala.

Tujihukumu sisi wenyewe kulingana na Neno la Mungu ili tukaweze kupona. Ruhusu nuru Yake kuangaza mioyoni mwetu na kufichua dhambi yo yote iliyomo maishani mwetu na tuweze kuupokea msamaha na kuoshwa.

## **Ni wakati wa kurudia matendo ya kwanza!**

Yesu alisema katika **Yoh.12:32**, **“Nami nikiinuliwa juu ja nchi, nitawavuta wote kwangu. Aliyanene hayo akionyesha ni mauti gani atakayokufa”** alikuwa akizungumzia habari ya Kusulubiwa Kwake (a.33). ni wakati gani Yesu anainuliwa na Wanafunzi Wake? Tunapokuja Mezani na kushiriki mkate na divai! Wakati mwangi hatujazingatia uwezo uliomo katika Meza. Tunastahili kumkumbuka Yesu katika Mauti Yake na Ufufuo Wake. Tumtazame Mwana Kondoo wa Mungu aliyezichukuwa dhambi za dunia na bado anafanya hivyo leo nafsi zinapoendelea kuja kwake Mungu kwa njia Yake.

# **HAKIKISHO LA WOKOVU WA SAYUNI**

## **NAFASI YA KUDUMU KATIKA MAOMBI KULINGANA NA NENO LA MUNGU ISAIAH 62**

**MUNGU ANANENA**

### **Isaya 62: Aya ya 1:**

*“Kwa ajili ya Sayuni sitanyamaza, kwa ajili ya Yerusalem sitatulia, hata haki yake itakapotokea kama mwangaza, na wokovu wake kama taa iwakayo.”*

### **Ni nani anayenena mahali hapa?**

Mungu ananena na nabii. Mungu anasema, “sitanyamaza.” Mungu ananena kwa njia ya unabii, akifichua kusudi Lake. Kusudi la Mungu ni haki na wokovu kupitia kwa kanisa. Hili ndilo anatakuja kutimiza.

### **HAKI NA WOKOVU**

**Haki inatangulia wokovu!** Yesu Kristo ni haki ya Mungu. Tayari amekuja (*Yer. 23:6: Yehova Tsidkenu –BWANA HAKI YETU atakuja.) 2 Kor. 5:21 “Maana alimfanya yeye asiyejua dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili tufanyike haki ya Mungu kwa njia yake Yeye.”*

**Haki yake itatokea kama mwangaza.** Tumetumwa kumhubiri Yesu Kristo. Petro, Siku ya Pentekoste alimnukuu nabii Yoeli akisema kuwa Siku za mwisho nitamimina Roho yangu juu ya wote wenye Mwili. Moja ya ishara ni wana wenu na binti zenu watatabiri. Huu unabii ni ushuhuda wa Yesu (*Ufu.19:10b*). Kila muumini atatabiri juu ya Yesu. Kila muumini atanena juu ya Yesu kwa nguvu za Roho Mtakatifu.

### **Wokovu ni “kama taa iwakayo” : inaweza kuonekana**

*Isa.60: 1 “Ondoka, uangaze; kwa kuwa nuru yako imekuja! Na utukufu wa BWANA umekuzukia.”* Nuru imekuzukia na utukufu wa Mungu uko juu yako.

### **Isaya 62: Aya ya 2a:**

*“Na mataifa wataiona haki yako, na wafalme wote watauona utukufu wako; nawe utaitwa jina jipy, litakalotajwa na kinywa cha BWANA”. [fananisha na. Isa. 60:3]*

Mataifa, kuwakilisha wale ambao hawajaokoka, **wataona** haki yako na wafalme **wataona** utukufu wako. Watavutiwa na hii nuru, hii inatuonyesha haki ya Mungu na utukufu. Ni kusudi la Mungu kuwa wote waokoke na wamjue Mungu.

**2Timoteo 2: 1-4:** Tuwaombee watu wote na wafalme na wote waliokwenye mamlaka.

**Matt. 6:10:** Tuombe “*Ufalme wako na uje!*”

### **JINA JIPYA**

### **Isaya 62: Aya ya 2b:**

*“Nawe utaitwa jina jipy, litakalotajwa na kinywa cha BWANA.”*

*Ufu. 2:17: “... jina jipy...” Ufu. 3:12: “ni jina jipy la BWANA”*

Katika itikadi zingine ni kwamba katika ndoa, mke anachukua jina la mme wake (**Yeremia 23: 6; 33:16**). Vivyo hivyo tunastahili kulichukua jina la BWANA wetu. Hatushahili kujivunia majina ya makanisa yetu au mkubwa wetu au jina lingine, bali uzalendo wetu kwa Yesu Kristo na kanisa Lake. BWANA amejitolea kulikamilisha kanisa Lake. (**Efe. 5:26-27**)

**“Nuru yenu na iangaze ... wamtukuze Mungu” (Matt. 6:16).** Baba anatukuzwa wakati watu Wake wanapong’aa na nuru ya wokovu kwa njia ya Roho Mtakatifu juu yetu. Watu wanapookoka kikweli, uwepo wa BWANA unaonekana maishani na kuonekana.

## KILEMBA CHA KIFALME

### Isaya 62: Aya ya 3:

**“Nawe utakuwa taji ya uzuri katika mkono wa BWANA, na kilemba cha kifalme mkononi mwa Mungu wako.”**

Taji ya uzuri: Kilemba (*kipande cha nguo kinachofungwa kichwani*):- *kilitumiwa na makuhani wakuu*.

Mkono: njia ambayo kazi itakamilishwa; nguvu, uweza.

- *msamiati: kukimbilia mkononi mwa, kuokolewa mikononi mwa*
- *“yadah” maanisha kushukuru, sifa, linatokana na neno la kiebrania kumaanisha “kuinua mikono juu”.*

Ikiwa kilemba cha uzuri hakizungumzii kitambaa alichovaa kuhani mkuu, kuna picha hapa ya Mfalme na Kuhani. Hii inazungumzia “*ukuhani wa wote waaminio*” (*Ufu. 1:6*) mfano wa ukuhani ambao Yesu ametutengenezea: kwa mfano wa Melkizedeki. Ni kupitia kwa mfano huu wa makuhani ndio Mungu anauonyesha utukufu wake na kufunika ulimwengu wote jinsi alivyoahidi (*Hesabu 14:21*). Kwa maneno mengine, tunatumwiwa na BWANA kumuangaza jinsi alivyo.

## TUNAITWA KUZAA SANA – WANA WENGI!

### Isaya 62: Aya ya 4:

**“Hutaitwa tena Aliyearchwa, wala nchi yako haitaitwa tena, Ukiwa; bali utaitwa Hefsiba; na nchi yako Beula; kwa kuwa BWANA anakufurahia, na nchi yako itaolewa.”**

Hii picha inaonyesha mabadiliko ya ajabu ambayo yanakuja juu ya watu wa Mungu. Hawataachwa na kuwa ukiwa tena bali wataolewa, ukifurahia wema wa Mungu. Hii ni picha ya kile ambacho Mungu pamoja na Yesu wanafanya kanisani ulimwenguni kote sasa. Kanisa liko linakubali, kuwa Bibi arusi; linatoka katika ukiwa, katika kuachwa. Tumaini jipyga na la hakika linachipuka. Tumaini la utukufu! (*Col. 1:27, Efe. 5:22-32*)

### Isaya 62: Aya ya 5:

**“Maana kama kijana amwonavyo mwana mwali na kufurahi, ndivyo wana wako watakavyokuoa wewe”**

- bila ndoa hakutakuwa na mazao, hakuna uhalali. Mungu analiambia kanisa hapa. Tunapomjua Mwana jinsi Anavyotujua, tutawazaa watoto wengi.
- Ndoa ni agano. Matunda ya agano letu (ndoа) na Mungu ni wana wengi waaminifu.
- *Ebr. 2:10* Yesu anazaa sana; Anawaleta “*wana wengi*” utukufuni.  
**“na kama vile bwana arusi amfurahiavyo bibi arusi, ndivyo Mungu wako atakavyokufurahia wewe.”**
- tunachukulia mipango na makusudi ya Mungu hivi hivi kwa ajili ya watu wake. Anatuita katika uhusiano wa agano ambao utazaa sana na kutufanya tuongezeke sana.

## Mungu ametuandalia nini?

**Efeso 1:17-19** – tumaini, wingi wa utukufu wake, mamlaka!

**Efeso 3:16-21** – uwezo, upendo, ukamilifu wa Mungu katika watu wake.

## MWITO WA MAOMBI

### ***Isaya 62: Aya ya 6:***

**"Nimeweka walinzi juu ya kuta zako, Ee Yerusalem; hawatanyamaza mchana wala usiku; ninyi wenyewe kumkumbusha BWANA, msiwe na kimya."**

Walinzi: Shamar, uwa (wa miiba) [Hosea 2:6] mlinzi, kulinda, wana;- onya, kulinda, kuweka, chunga, kupokea, kuokoa, kungojea, mwanga (lizi).

**Ezekieli 3:17** "...mlinzi wa nyumba ya Israeli ... ukawape maonyo haya yatokayo kwangu"

Tunajua ujumbe – ni watu wangapi **hatujaonya**?

**Aya ya 17-21:** waonye waovu; waonye wenyewe haki.

**2 Thesalonike 1:8,9** Wale wasiomjua Mungu na wale wanaijua injili lakini hawaitii watahukumiwa.

**Isaya 52:8-12** Bwana anairejesha Yerusalem. Analikusa kanisa Lake duniani.

**Yeremia 6:17 Ezekieli 33:1-11** Mlinzi alikuwa akiwaonya watu kuisikia tarumbeta, yaani, Neno la Mungu. Wale wasioisikia na kuitii, hukumu itakuja. Maombi yanatakikana kuwa kwa msingi wa Neno la Mungu kwa sababu ni mapenzi ya Mungu.

Ulinzi lazima uwe mchana na usiku.

### **Na nani?**

Mungu anatafuta watu waombezi watakaoweka uwa wa kuwazingira watu kwa maombi (kama Hosea alivyo mwekeea mke wake, **Hosea 2:6**)

- Ni nani atakayelilinda kundi katika maombi
- Ni nani atakayelinda watu wa Mungu katika maombi
- Ni nani atakayeshughulikia mahitaji ya mwingine katika maombi
- Ni nani hatamwacha akae kimya mpaka ...

### ***Isaya 62: Aya ya 7:***

**"Wala msimwache akae kimya, mpaka atakapoufanya imara Yerusalem, na kuufanya kuwa sifa duniani."**

## KWA MSINGI WA NENO LA MUNGU

Mungu amejitolea mwenyewe katika **aya ya 1-2**. Sasa tufanye sehemu yetu: bila kukoma, kudumu, maombi ya kujitolea. Tusimwache akae kimya. Mungu atatimiza kwani njia ya watu wake wasiomwacha apumzike mpaka afanye.

**Lengo:** kanisa la Yesu Kristo, liwe sifa kwa watu wote.

Angalia baadhi ya mienendo ya hili kanisa.

**Efeso 1:3-6; Efeso 1:7-12; Efeso 1:13-14**

Kanisa la aina hii ni la utukufu wa sifa zake.

Walinzi wasichoke – lakini wadumu katika maombi hadi tupate kile amesema atatupatia, sio kile tunataka. Tambua mahali pa maombi, maombezi, kunena maombi, hata labda kwa hasira, maombi ya vujo. (**Matt. 11:12**)

Tunashughulikia mioyo. Bwana Yesu Kristo anawaalika wote ambao wanataka kuwa sehemu ya Jeshi la kuwaleta watu au mavuno ghalani.

## TUTASHANGILIA KATIKA WAKATI WA MAANDALIZI

### Isaya 62: Aya ya 8:

*“BWANA ameapa kwa mkono wake wa kuume, na kwa mkono wa nguvu zake, hakika sitawapa adui zako nafaka yako tena kuwa chakula chao; wala wageni hawatakunywa divai yako uliyoifanyia kazi.”*

### Isaya 62: Aya ya 9:

*Lakini walioivuna, ndio watakaoila, na kumhimidi BWANA; na walioichuma ndio watakaoinywa, ndani ya nyua za patakatifu pangu. [mazao/chakula nyumbani]”*

Huduma zetu hazitanyang'anya tena; hatutasumbuka tena, matunda yetu hayatapukutishwa.

**Divai mpya ni Roho** – furaha katika Roho Mtakatifu. Njooni na mnywe mshibe.

*Isa. 55:1 Yoh. 7:37-39; Ufu. 22:17*

## NI NANI ATAKAYETENGENEZA NJIA?

### Isaya 62: Aya ya 10:

*“[Piteni, piteni, katika malango! Itengenezeni njia ya watu; tutieni, tutieni barabara; toeni mawe yake [mambo yanayowakwaza watu]; Twekeni bendera kwa ajili ya kabila za watu.”*

Jeshi ka Gidioni lilipata fursa ya kuokoa taifa zima. Wanajeshi 10,000 walikunywa maji mtoni, lakini kulikuwa na mtihani kwenye mto. 300 tu ndio walioupita mtiani. 300 tu ndio waliosikia kile Mungu alikuwa akisema, na kutii.

Mto wa Bwana unatiririka, na wengi wamekuja kunywa mtoni, lakini wamegeuka na kurudi. Mungu anatuita tutengeneze njia. Piteni katika malango. Malangoni ni mahali pa mamlaka. Mungu anawaita watu ambao watapita katika malango na kukomboa mataifa yote kutoka gizani, kuwatengenezea watu njia. Mungu kila wakati anawaita watu ambao wako tayari kukomboa ulimwengu, na kuharibu ngome zote za muovu, na kuomba na kuingia katika mataifa, mijji, vijiji.

## BWANA YUAJA

### Isaya 62: Aya ya 11:

*“Tazama BWANA ametangaza habari mpaka mwisho wa dunia, Mwambieni binti Sayuni, Tazama wokovu wako umekuja; Tazama dhawabu yake i pamoja Naye, na malipo yako mbele zake.”*

Aya hii inazungumzia juu ya Kurudi Kwake Yesu mara ya Pili. Kanisa linaambiwa kijiandaa sasa. Yesu anakuja na dhawabu yake mkononi na malipo yako mbele zake.

KANISA! Hakika wokovu wako umekaribia! Tazama yuaja!

Wakati ni mfupi – Mwenye haki yu mlangoni (*Yakobo 5:9*). Tumia kila nafasi kuhubiri injili ya wokovu.

## KANISA LIKO LINAKAMILISHWA

### Isaya 62: Aya ya 12:

*“Nao wataitwa, watu watakatifu, waliokombolewa na BWANA; Nawe utaitwa, Aliyetafutwa, Mji usioachwa.”*

Watu wa dunia watalitambua kanisa linapochipuka kama kanisa tukufu.

## TAMATI

Swali la ajabu ambalo unaweza kuulizwa ni “nitawezaje kupata kuokoka?” Mungu ametengeneza njia. Sio mapenzi yake ye yote apotee. Tumeitwa ili tudumu katika maombi na tutii Neno Lake.

Lengo ni uinjilisti wa ulimwengu mzima (*Matt. 28:18-20*), kumhubiria kila mtu (*Marko 16:15*). Hatutapumzika hadi, kanisa, limetimiza Tume Kuu.

Jinsi ilivyo mizuri  
Juu ya milima  
Habari njema  
Aletaye habari njema,

miguu yake yeye ailetaye,  
yeye aitengenezaye amani,  
yeye autangazaye wokovu

Aumbiaye Sayuni, "Mungu wako Anamiliki!"

Isaya 52:7

# **WOKOVU KWA MATAIFA**

## **“NYUMBA YANGU ITAITWA NYUMBA**

### **YA MAOMBI KWA MATAIFA YOTE”**

#### **FUNDISHO KUTOKA KWA ISAYA 56:1-8**

##### **KATIKA AGANO JIPYA**

Katika **Matt. 21:13**, Yesu ananukuu kutoka kwa **Isa. 56:7** baada ya kuwafurusha **wafanyabishara (aya ya 12)**. Halafu katika **aya ya 14**, "vipofu na vilema wakaja kwake hekaluni, na akawaponya". Wakati hekalu liliposafishwa na kutangazwa kuwa Nyumba ya Baba kama alivyokusudia, mara kukawa na maombi kwa ajili ya vipofu na vilema na wakaponywa! Kanisa likaanza kufanya kazi kama lilivyokusudiwa, kulingana na Neno la Mungu.

Hata hivyo, kulikuwa na upinzani kutoka kwa wakuu wa makuhani na waandishi (**aya ya 15-16**). Wakati wo wote ambapo watu wa Mungu waliamka na hamu ya kurudia Ukristo wa Agano Jipyä na kuchukua hatua hadi mwisho, kutakuwa na upinzani mzito na upofu kwa matendo mema kutimizwa kwa njia ya nguvu za Roho Mtakatifu.

Kutimiza kusudi la Mungu kulingana na Maandiko Matakatifu tunakabiliana na mabadiliko yanayoendelea. Sera za dini na mitindo ya dini na utawala, na swala nyeti la jinsi tunavyofanya kile kinaitwa ‘kanisa’, hatutaona vipofu na vilema wakiponywa.

##### **JE! KANISA LAKO NI NYUMBA YA MAOMBI**

**Nyumba yangu itaitwa nyumba ya maombi:** kwa kiwango gani, ikiwezekana, je! Kanisa lenu ni nyumba ya maombi?

Mara tu watu wa Mungu watakaporudia kudumu katika maombi, maombi ya kujitolea kulingana na Neno la Mungu, tutaona wingi na wingi wa miujiza kutoptana na maombi yaliyojibowi.

**Yohana 15:7-8:** Yesu alisema kuwa tukikaa ndani Yake na maneno Yake [rhema – neno lililohuishwa, kusikia kwa imani **Rum. 10:17**] yakae ndani yetu, tutaomba cho chote tutakacho na tutatendewa. Kwa hili Baba anatukuzwa, tutazaa matunda mengi ambayo ni wanafunzi wake hakika. Maombi ni ufunguo wa matunda mengi; maombi ni njia ya kufanya wanafunzi.

##### **WOKOVU KWA MATAIFA**

**Isaya 56:1** “*Shikeni hukumu, mkatende haki, kwa maana wokovu wangu u karibu kuja, na haki yangu kufunuliwa.*”

Haki ya Mungu ilifunuliwa katika Mwana Yesu Kristo; Wokovu wa Mungu ulitufikia kwa njia Yake Kristo, ili ye yote amwminiye aweze kuokolewa.

**Isaya 56:2:** “*Heri afanyaye haya, na mwanadamu ayashikaye sana; azishikaye sabato asizivunje, auzuiaye mkono wake usifanye uovu wo wote.*”

Nani anafanya nini? Ashikaye nini? - mtu amwaminiye Yesu Kristo kwa ajili ya wokovu Wake na kumtumainia kwa ajili ya haki.

Pia ”*azishikaye sabato asizivunje, auzuiaye mkono wake usifanye uovu wo wote.*” Mungu anawatafuta watu watakatifu, bila lawama au hila. Ikiwa tunatamani kurithi wokovu wake mkamilifu, ikiwa tunatamani kuvikwa katika vazi la haki, kunahitajika kujitolea kwa moyo wote katika Neno Lake na njia Yake.

## MTU ATAWEZAJE KUJIZUIA KUZIVUNJA SABATO?

Amri ya nne inasema "Kumbuka Siku ya Sabato na uiweke takatifu." (*Kutoka 20:8*) Mara nyingi katika Agano la Kale, watu wa Mungu waliadhibiwa kwa sababu ya kukosa kuitakasa Sabato. Je, hili fundisho la maana linakamilika aje katika Yesu Kristo?

**Kutoka 20:11:** "Maana kwa siku sita BWANA alifanya mbingu na nchi, na bahari, na vyote vilivymo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya sabato akaitakasa."

**Mwanzo 2:2-3:** "Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. Mungu akaibariki siku ya saba katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya."

## KUSTAREHE KWA MUNGU

Mungu mwenyewe aliitenga siku ya saba na kuibariki, kuifanya kuwa maalum Kwake na kwa viumbe vyote. Katika **Kutoka 20:11** Musa anasema "pumziko" la Mungu, akinukuu kutoka Mwanzo. Mungu aliitenga sabato kwa kustarehe Kwake na anaalika viumbe vyake vyote, kuingia katika pumziko hilo.

Siku sita za uumbaji zilikuwa na jioni na asubuhi, kuikamilisha siku. Hakuna mahali pametajwa kuhusu siku ya saba kuwa na jioni na asubuhi. Hili linatufundisha kuwa hiyo ni **siku ya milele**, Siku ya Mungu, siku ya maalum sana na kamilifu!

**Kolosai (2:16-17)** yafundisha kuwa sabato na mwandamo wa mwezi na kadhalika vilikuwa mifano ya Yule alikuwa anakuja – Kristo, ambaye ndiye hakika. Kristo ni Mwana wa milele wa Mungu, Mpendwa, hakuumbwa. Ametoka mbinguni na kupitia kwa ufuluo wake ameshinda mauti na hivyo ameshinda vizuizi vya ulimwenguni, akituleta kwenye "pumziko la Mungu". Yeye ni muumbaji (*Yoh. 1:3*) ambaye anatutengenezea njia ya kuingia katika Pumziko la sabato ya Mungu; kupumzika kutoka kwa kazi zetu wenyewe (*Ebr. 4:10*). Kwa njia ya imani tumekuwa warithi pamoja na Kristo (*Ebr. 3:14*), na kwa njia ya imani tumewezeshwa kuingia katika pumziko Lake (*Ebr. 4:3,11*).



Mwana damu asili yake alilingia katika pumziko la Mungu siku ya saba lakini akaondoka katika pumziko Lake kwa sababu ya Dhambi [uasi]. Kwa imani (kutii) tunaingia katika pumziko la Mungu kwa njia ya Kristo na kazi yake aliyoimaliza. Kwa hivyo kuiweka sabato katika Agano Jipyaa ni kwa njia ya **imani, kutii na kukaa ndani ya Kristo**. Kila siku ni siku ya Bwana na tunatakipana kuwa watakatifu kwa Bwana kila siku.

## MWANA WA MGENI

**Isaya 56:3:** "Usiache mwana wa mgeni aambatanaye na BWANA aseme hivi, 'Hakika BWANA atanitenga na watu Wake';"

Mwana wa mgeni, ambaye si Myahudi, ambaye ni mwongofu ama pia yule ambaye hajapashwa tohara ambaye ameamin, anatakikana akubalike kikamilifu maana Bwana amemkubalia. Hata hivyo katika Agano Jipyaa, hakuna tofauti katika BWANA kati ya Myahudi na Myunani, bali ni mtu mmoja mpya.

## TOWASHI

**Isaya 56:3b** “Wala towashi asiseme, ‘mimi ni mti mkavu’ [akizungumzia hali yake ya kukosa kuwa na watoto; matowashi pia walitengwa kutoka kwa kusanyiko la Bwana chini ya sheria ya Musa (**Kumbu 23:1**)] kwa Maana BWANA awaambia hivi matowashi, wanaozishika sabato zangu, na kuyachagua mambo yanipendezayo, na kulishika sana agano langu. Nitawapa hawa nyumbani mwangu, na ndani ya kuta zangu, kumbukumbu na jina, lililojema kuliko kuwa na binti na wana; nitawapa jina lidumulo milele, lisilokatiliwa mbali’ (**aya ya 4,5**).

Ahadi hii ya Mungu ilitimia katika **Matendo 8:26-39**. Katika habari za Yule Towashi wa Kushi anayeokolewa na imani yake na kubatizwa. Tayari alikuwa ameaminu Mungu na alikuwa amejunga na njia ya kuabudu Mungu ya Wayahudi. Mungu amempa towashi jina katika Neno Lake ambalo litadumu milele!

## WANA WA MGENI

**Isaya 56:6** sio tena mwana, mmoja, bali “wana”, kumaanisha wengi.

“wana wengi wa mgeni” wanaoambatana na Bwana.

“kulipenda Jina la Bwana” (ye yote atakayeliitia jina la Bwana ataokoka, **Yoel 2:32, Rum 10:13**),

“kuwa watumishi wake” – Yule ambaye anaiiweka sabato ikiwa takatifu (aliye mwaminifu kwa "pumziko" katika Kristo, akimwabudu Mungu kwa roho na kweli)

“na kulishika sana agano langu” (**Matt. 28:20** “kuwafundisha kushika yote niliyowaamuru ninyi”) -

**Isaya 56:7** “Nitawaleta hao nao katika mlima wangu mtakatifu,”

(Sayuni ni mlima Mtakatifu; ni nani awezaye kuupanda mlima wa Bwana? angalia **Zab. 15** na **Zab. 24:3-6**)

“Na kuwafurahisha katika nyumba yangu ya sala; ” (kanisa, Nyumba ya Mungu ni nyumba ya maombi; “kwa kuwaleta mataifa wengi katika nyumba Yake” (**angalia Isaya 2:1-3 na Mika 4:1-3**)

“Makafara yao na dhabihu zao zitakubaliwa juu ya madhabahu zangu”;

Makafara na dhabihu ni nini? Angalia **Walawi Sura ya 1 - 7**. Yesu Kristo alijitoa mwenyewe kama kafara kwa ajili ya dhambi zetu mara moja siku zote, kutimiza haki yote ya sheria(Ebr. 10:12). Tunapomjia Mungu kwa imani katika Kristo, tukitambua kafara yake ya kifo msalabani na kutubu na kukiri dhambi tunasamehewa, tunatakaswa na kukubaliwa na Bwana Mungu.

“Kwa maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya maombi kwa mataifa yote”

Nyumba ya Mungu ni kanisa (**Efe. 2:19-22, Ebr. 3:1-6**).

Kanisa ni nyumba ya Mungu kwa mataifa yote; injili inatakiwa ihubiriwe kwa mataifa yote; kuhubiri injili kwa bidii hadi ishara na maajabu yaanze na kudumishwa na maombi.

**Isaya 56:8** “BWANA Mungu akusanyaye waliofukuzwa katika Israeli akasema, Pamoja na hayo nitamkusanya na wengine, zaidi ya hao walio wake waliokusanya.”

Mungu siku zote amekusudia kuwakusanya watu kutoka katika kila taifa, kabilia, lugha. Neno lake kila mara linazungumzia juu ya kusudi lake la milele katika Kristo.

Katika sehemu hii ya Isaya tunamwito mkuu kutoka kwa Neno la Mungu la kurudia Maombi. Maombi yalikuwa sehemu ya matendo ya kwanza ya kanisa katika kitabu cha Matendo (**Matendo 2:42**). Yesu alituonyesha mfano wa jinsi alivyojitlea katika maombi. Alisema, “sifanyi lo lote ila lile ninaliliona Baba akifanya.”

Sasa hivi Bwana analiita kanisa Lake kuomba na uinjilisti. Uinjilisti hutokana na maombi. Sasa hivi Mungu anainua watenda kazi na kuwatuma katika mavuno. Wale ambaa wanafaulu

sana ni wale ambao wana ngome ya maombi. Mungu pia anawaita watu kwa njia kuu katika ufalme wake. Watu ambao wamejua tu njia ya kuabudu ya Budha ama ya kiislamu, wameanza kupokea na kutembelewa na Bwana kwa njia kuu. Yesu anawatokea watu katika maono na kuwafunulia kuwa Yeye ni Nani.

## **KAZI YA KUFANYA**

1. Chukua mda wakujitakasa mbele ya Mungu, kabilii dhambi, uvuguvugu na cho chote kilicho kizito juu yako sasa.
2. Chukua wakati katika nyumba yake, yaani, katika uwepo wake ukimsifu na kumuabudu Mungu.
3. Chukua wakati uombee mataifa! yaani watu wasiomjua Mungu, waite waje kwa Yesu Kristo! Itisha rehema za Mungu juu ya waliopotea!

## TUME KUU

### MPANGO WA UINJILISTI

*Matt. 28:18-20 “Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika Jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari’.”*

Katika **Matt. 24:14** Yesu anatoa ufupisho wa Tume Kuu: “*Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.*”

**Marko 16:15-20** ananukuu Tume kuu tena Great. **Aya ya 16** inawalaani wale ambao wanasikia bali hawaamini. **Aya ya 17 na 18** inanena juu ya ishara zitakazowafuata waaminio: “... katika jina Langu watatoa pepo wachafu; watanena kwa lugha mpya, watawashika nyoka; na wakinywa cho chote cha kuvisha, hakitawadhuru kamwe; watawawekea wagonjwa mikono juu yao, nao watapata kupona.”

Maandiko Matakatifu yanaendelea kusema katika **aya ya 20**, “*Nao wale wakatoka, wakahubiri kote kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile Neno kwa ishara zilizofuatana nalo*”. Bwana ndiye anayelithibitisha Neno kwa isara na maajabu.

**Luka 24:44-49** Luka anaandika kuhusu Tume Kuu. **Aya ya 44** inasema kuwa “*ni lazima niyatimize yote niliyoandikiwa katika Torati ya Musa, na katika manabii na Zaburi.*” Mengi ya mambo haya bado hayajatimia.

**Zab. 2:8:** “*Uniombe, nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako na miisho ya dunia kuwa milki yako.*”

**Zab. 110:1** “... *Hata niwafanyapo adui zako kuwa chini ya miguu yako.*”

Huu unabii bado haujatimia.

**Luka 24:47:** “... *toba na ondoleo la dhambi lihubiriwe katika jina lake katika mataifa yote...*”

Huu ni ujumbe wa injili ambao utahubiriwa kwa mataifa yote, ya kwamba dhambi zimesamehewa na kuondolewa. Mamlaka haya pia aliwapa wanafunzi (**Yoh. 20:23**).

Mataifa yanatakikana kupokea ujumbe wa injili. Kila mtu binafsi apokee ujumbe wa injili. Ufalme wa Mungu unakua mmoja kwa mmoja, nafsi kwa nafsi.

#### **Kubeba ushahidi**

Kuwaambia watu juu ya Yesu sio kubeba ushahidi wa injili. Kubeba ushahidi kunaonyesha kuwa kuna kitu cha kuonyesha - ushahidi.

Kunatakiwa kuwe na **ushahidi wa nguvu** pamoja na Neno. Watu wataona nini?

Katika **Matendo 8:17-19** Simoni aliona kitu kikitendeka wakati mitume walipo wawekea watu mikono. Alitoa pesa ili anunue hizo nguvu.

**Luka 7:18-22:** Yohana Mbatizaji alituma wajumbe kwa Yesu akiuliza , “*Wewe ndiwe Yule ajaye, au tumtazamie mwengine?*” Ndipo Yesu alipowajibu “*Nendeni mkamwambie Yohana hayo mliyoyaona na kuyasikia; vipofu wanapata kuona, viwete wanatembea, wenye ukoma wanatakasika, na maskini wanahubiriwa habari njema.*”

Lazima kuwe na ushahidi wa injili, ushahidi wa nguvu za unjili.

**Matendo 1:8** inaahidi nguvu kuwa ushahidi. Mitume katika kanisa la kwanza waliona hizo nguvu zikitenda kazi. **Matendo 14:3:** “... *Bwana ... aliye shuhudia Neno la neema Yake, akiwajaalia ishara na na maajabu yatendeke kwa mikono yao...*”

**Marko 16:17** inasema “*ishara hizi zitawafuata waaminio*”. Ushahidi wa Neno ambao umenenwa utakuwa kwamba mapepo yanatolewa, watu wanana na lugha mpya, watu wanashika nyoka na kunywa sumu lakini hawatadhurika na wagonjwa wanaponywa.

**1 Kor. 4:20:** “*Maana ufalme wa Mungu sio kwa maneno tu bali Kwa nguvu.*”

**1 Kor. 2:1-5** Paulo alikuja na kudhihirisha Roho na nguvu, ili imani isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.

**Rum 1:16-17** Injili ni nguvu za Mungu ziletazo wokovu.

**1 Kor. 1:18** kuhubiri kwa msalaba ni nguvu za Mungu.

**Rum 15:18-19** Mataifa walihubiriwa injili kwa ishara kuu na maajabu.

Injili bila ishara na maajabu ni injili ambayo haijakamilika.

**Ebr. 2:4:** “*Mungu naye akiwashuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda Mwenyewe.*”

Yesu alitiwa Mafuta na Roho Mtakatifu na nguvu na akatenda miujiza mingi, na ishara na maajabu (Matendo 2:22;10:38).

Tusipokuwa na upako wa Roho Mtakatifu na nguvu, tutajuje kama Mungu yuko pamoja nasi? Yesu alimwambia Nikodemo, “*Amini, amini nakwambia, twanena tukijuacho na kushuhudia kile tumeona, na hampokei ushuhuda wetu.*” (**Yoh. 3:11**)

Katika **Yohana 14:11** Yesu anasema, “*Mnisadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba na Baba yangu ndani yangu, la! hamsadiki hivyo, sadiki kwa kazi zenyewe.*” Pia akasema katika **Aya ya 12** Kuwa ye ye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, ye ye naye atazifanya, na kubwa kuliko hizo.

### **Yesu yuko wapi Leo?**

Yuko anaandaa mavuno makubwa na kuwaita watenda kazi katika mavuno.

**Yohana 15:14** Tukimpenda Yeye tutazishika amri zake.

**Yohana 15:16** Alituchagua ili tumzalie matunda yatakayo dumu.

**Yohana 17:18** Ametutuma ulimwenguni.

**Yohana 17:20** Yesu anaomba kuwa wengine wataliamini Neno la Mungu.

**Ebr. 4:12** inatwambia Neno la Mungu linafanana aje. Li hai na lina nguvu, lina makali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena la choma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kutambua mawazo na makusudi ya moyo.

### **MFANO WA YESU**

**Matt. 3:15** Yesu alibatizwa kutimiza haki yote. Mungu anahitaji nini kutoka kwako?

**Matt 3:16** Roho Mtakatifu akamjilia.

**Matt. 4:1** Yesu aliongozwa na Roho kwenda nyikani kujaribiwa na shetani.

**Rum. 8:14** inatwambia kuwa sisi ni watoto wa Mungu; Roho wa Mungu atatuongoza jinsi alivyomuongoza Yesu.

**Matt 4:11** Yesu alishinda na akahudumiwa na malaika – tarajia usaidizi wa malaika!

**Luka 4:14:** Yesu alirudi kutoka nyikani katika Nguvu za Roho Mtakatifu.

**Matt. 4: 23-24:** Yesu alienda kote akifundisha, akihubiri, akiponya kila aina ya magonjwa na maradhi na wale waliosetwa na mapepo wachafu.

### **Ni kitu gani kingine Yesu alifanya?**

1. Aliwafundisha mitume kumi na wawili; watatu wakipokea mafunzo maalum. *Ni nani anakufundisha wewe?*
2. Aliwajenga wale sabini na kuwatuma kama watenda kazi kuhubiri, kuponya na kutoa pepo wachafu. (*Luka 10*)
3. Alikuwa katika uhusiano wa uchungaji na watu zaidi ya mia tano (*1 Kor.15:6*).
4. Yesu alisafiri kila mahali. *Marko 1:38, Yohana 6:15*. Hakuwacha kutawaliwa na mwanadamu.
5. Kila wakati aliambatana na wanafunzi wengi. Hakuhudumu pekee yake.
6. Alikuwa na wanawake katika kundi Lake waliomhudumia na kusimama na huduma Yake. (*Luka 8:1-3, Matt. 27:55*)
7. Alitumwa kwa wanakondoo wa nyumba ya Israeli waliokuwa wamepotea (*Matt. 10:6*). Amri yake kwa wanafunzi ilikuwa waende Yerusalem, Uyahudi, Samaria na miisho ya dunia yote (*Matendo 1:8*).

Tumetumwa katika kila kijiji, kila mji, kila kichochoro, kila eneo la mashambani.

### **TUME KUU KATIKA AGANO LA KALE**

Kutajwa kwa mara ya kwanza ni katika *Mwanzo 1:26-28*. Mungu alimwambia Adamu na Hawa kuijaza nchi yote. *Efeso 2:10* inatuonyesha kuwa sisi ni viumbe vipya vyta kukamilisha tume hiyo waliyopewa Adamu na Hawa.

**Zaburi 2:6-12** inazungumzia juu ya kuomba nafsi kama urithi wetu na miisho ya dunia kama milki yetu.

**Zaburi 110:1-3 na 5-6:** Bwana atayahukumu mataifa.

Mataifa na Wayunani ni wale wasiomjua Mungu.

**Isaya 2:2-3:** Mungu atawaita Mataifa. Huu unabii unarudiwa tena katika *Mika 4:1-3*.

**Isaya 49:1 na 7-9:** Waliofungwa wanaambiwa “*Haya, tokeni*”. Tunatakikana kutoka katika upako na kuwambia wale wasiomjua Mungu, “Haya, kujeni, jinyosheni, hamna haja tena ninyi kuishi katika hofu, tokeni kwenye giza!”

**Isaya 49:9-12:** Bwana atawaongoza na kuwatangulia na kuwaita kutoka mbali.

Strong's Concordance, 'sinimu' ni sehemu ya mbali kule mashariki. Mungu anaita Uchina

**Isaya 55:5:** Tuwaite mataifa.

**Isaya 60:7** Makundi yote ya Keda na kondoo waume wa Nebayothi wanaitwa katika nyumba ya Mungu – hawa ni wana wa Ishmaeli.

Huu ndio wakati wa kupanda Makanisa. Sasa ni wakati wa kutoa ushuhuda katika kila kundi la watu.

**Isaya 56:7-8:** Bwana anasema, “*Nyumba yangu itaitwa nyumba ya Maombi kwa mataifa yote.*”

### **Matokeo yatakuwa nini tukiwa na ushahidi wa nguvu kila mahali?**

Wale wanaaoamini watafanya kanisa ambalo litafaulu. Kanisa litadumu katika mafundisho, ushirika, kuumega mkate na kusali (*Matendo 2:42*). Tarajia ishara na maajabu na Bwana kuongeza kwa kanisa kila siku wanaookoka(*Matendo 2:43-47*).

**Hagai 1:14:** Mungu aliichochea Roho wa Zerubabeli kuijenga tena Nyumba ya Bwana.

**Zekaria 4:6-10:** Usiidharau siku ya mambo madogo.

**Inawezekanaje? Efeso 4:11-12**

Mitume na Manabii ni msingi wa kanisa la Agano Jipya. Ili kanisa likue Mchungaji, Muinjilisti na Mwalimu wanahitajika kujenga katika huduma ya msingi ya Mtume na Nabii.

Lengo ni utimilifu na kukomaa. Mwili wote ukihudumu, kila sehemu ikiungamanika na kushikamana vizuri na kuchangia katika kuujenga Mwili katika upendo.

Sasa hivi tunaingia katika wakati mkuu wa mwisho wa mavuno. ***Yohana 4:35*** inasema mashamba yako tayari “*meupe tayari kwa mavuno*”. ***Matt. 9:37-38*** anatwambia “*mavuno ni mengi, bali watenda kazi ni wachache. Kwa hivyo ombeni Bwana wa mavuno awatume watenda kazi katika mavuno Yake*”.

Mungu anawaita watu sasa kuinuka kwa moyo wao wote katika kujitolea kutimiza Tume Kuu.

***Matt. 24:14:*** “*Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.*”

# **KUINGIA KATIKA MILANGO YA MJI**

## **MTAKATIFU**

*"ULIKUWA NA MILANGO KUMI NA MIWILI; NA MAJINA YAMEANDIKWA AMBAYO NI  
MAJINA YA KABILA KUMI NA MBILI ZA WAISRAELI"*

*Ufunuo 21:12*

Yohana tayari alikuwa ameona mji "*mji mkubwa, mtakatifu, Yerusalem, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mwenyezi Mungu*", **aya ya 10**, "*wenye utukufu wa Mungu*", **aya ya 11**, na alikuwa amejulishwa kuwa mji huu "*ni Bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo*", **aya ya 9**.

Milango ni mahali pa kuingilia! Mtu hawezi kukwea kwenye ukuta. Wevi na wanyang'anyi hawawezi kuingia katika mji Mtakatifu. (**Yoh. 10:1**).

Yesu akasema, "*Mimi ndimi mlango. Mtu akiingia kwangu, ataokoka, ataingia na kutoka na kupata malisho.*" (**Yohana 10:9**)


Milango katika miji ya zamani ilimaanisha mahali pa mamlaka: wazee walikaa malangoni na kufanya maamuzi kuwalhusu watu (**Ruthu 4:1-2**). Yesu alizungumzia juu ya "*milango ya kuzimu*" haitalishinda kanisa (**Matt. 16:18**); kanisa litashinda mamlaka na nguvu za kuzimu zinazowakilishwa na milango.

Ikiwa milango ni mahali pa kuingia, ni nini hufungua milango kumi na miwili ya mji mtakatifu? Je! Mtu anaweza kuingia kwa mlango wo wote wakati wo wote? **Ufu. 21:25** inasema kuwa milango yake haitafungwa kamwe mchana, kwa maana humo hamna usiku. Tunawezaje kuingia katika milango hiyo ya mji? "*Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo ndio hekalu lake*" (**Ufu. 21:22**). Kwa hivyo kuingia katika mji mtakatifu ni sawa na kuingia katika uwepo wa Mungu. Tunawezaje kuingia kikamilifu katika uwepo Wake?

Tukifuata mapangilio wa majina ya kabile za wanaisraeli alivyo zitabiria Yakobo katika **Mwanzo 49**, tutapata mtiririko kutoka kwa mlango mmoja hadi mwingine, kulingana na maana ya jina. Ni kama mlango wa kwanza unatufahamisha mlango wa pili, na mtiririko ni huo hadi ule mlango wa kumi na mbili.

Maana ya majina imechukuliwa kutoka kwa mstari wa Maandiko Matakatifu na Kamusi aina ya Strong's Concordance. Tafsiri ya majina katika unabii unatolewa kwa sehemu ya unabii wa maneno ya Yakobo katika **Mwanzo 49** na ya Musa katika **Kumbu 33**, na pia katika maandiko yote ya Biblia. Hili sio fundisho kamilifu bali ni utangulizi tu.

## MILANGO YA KUINGIA MJINI MTAKATIFU



## MLANGO WA KWANZA: REUBENI

Reuben maana yake ni “*tazama mwana*” ama “tazama, mwana” (*Mwanzo 29:32*). Reuben aliwa wa Kwanza wa Yakobo; yeeye ni mlango wa kwanza.

Wakati mtu anapomtazama Yesu, Mwana wa Mungu, na kumuamini anaokolewa. Mlano wa KWANZA ni wokovu. Mtu hawezi kuingia mji Mtakatifu hadi aokoke.

*Yoh. 14:6:* "Mimi ndimi njia, Kweli na Uzima. Hakuna ajaye kwa Baba ila kwa njia yangu mimi."

*Marko 16:16:* "Aaminiye na kubatizwa huyo ataokoka."

*Yoh. 3:16:* "kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwana wake wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee bali apate uzima wa milele."

Tunaingia mji mtakatifu Kwanza kwa njia ya wokovu: Tukimtazama Mwana! Ni lazima tuokoke kwanza ili tuweze kuingia katika ufalme wa Mungu (*Yohana 3:3*).

## MLANGO WA PILI: SIMEONI

Maana yake ni "*kusikia*", Mungu alimsikia Lea, (*Mwanzo 29:33*); kusikia. Mlango wa Pili unazungumzia juu ya kumusikiza Mungu; kuisikiza sauti Yake. Ili tumsikie Mungu vizuri tunahitaji kujazwa na Roho Mtakatifu.

*Yohana 14:26:* Atatukumbusha yote ambayo Yesu alitufundisha;

*Yohana 16:13:* "kile anasikia, atanena; na atawajulisha yale yatakayo kuja."

Tunaokolewa kuingia katika mlango wa kwanza; tunafanyika wenyeji wa mbinguni juu (*Filipi 3:20*); majina yetu yameandikwa kitabuni cha uzima. (*Ufu. 21:27*). Hata hivyo ili tuendelee na Bwana tunahitaji kujazwa na Roho Mtakatifu (*Matendo 1:8; 8:17; 9:17; 10:44; 19:6*).

## MLANGO WA TATU: LAWİ

Maana yake: *Kujiunga*, (*Mwanzo 29:34*). Roho Mtakatifu ambaye tumepokea, katika mlango wa Pili, anatubatiza katika Mwili wa Kristo (*1 Kor. 12:13*). Tunaunganika kwa mwili kama viungo (*aya ya 12*). Mara tunapojiunga na mwili, baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu, tunaanza kuhudumu; Lawi aliwa kabilia la kuhudumu chini ya Sheria ya Musa. (Tazama *Kumbu 33:8-11*: anaenenda katika vipawa vya Roho [Thumimu na Urimu]; anayaweka malengo ya Mungu juu ya malengo yake, *aya ya 9*; analifundisha Neno la Mungu, *aya ya 10*; Mungu anabariki mali zake na kumlinda, *aya ya 11*).

## MLANGO WA NNE: YUDA

Yuda ni neno la Kiebrania "yadah", linalomaanisha *kuinua mikono kwa sifa na shukrani*. Yuda linamaanisha sifa (*Mwanzo 29:35*). Yakobo alisema Yuda atasifiwa na ndugu zake (*Mwanzo 49:8*); ni kama mwana simba kutoka katika mawindo; atakuwa mtawala na mfanya sheria (*aya ya 9-10*). Mlango wa Nne wakuingia katika mji Mtakatifu ni Yuda: sifa kwa Mungu wetu. Watu ambao wakeokoka, wamejazwa na Roho Mtakatifu na kuungana pamoja kama mwili unaohudumu, unakuja kwa Bwana katika sifa na kuanza kutambua nguvu za sifa. Na tutoe ibada ya Sifa (*Ebrania 13:15*).

## MLANGO WA TANO: ZABULONI

Zabuloni maana yake ni makaazi, *makao*; Mungu anawashukia watu wa Sifa ama watu wa sifa wanapewa njia ya kuingia katika uwepo wa Mungu. Mungu "*Anaketi juu ya sifa za Israeli*" (*Zab. 22:3*); Mungu anakaa katika sifa (*Zab. 132:13-14*).

Kama makuhani wa Mungu tunajifunza kuja katika uwepo wake na kumhudumia; tunaingia katika mahali patakatifu pa Mungu pale Anakaa; tunakuja Sayuni (*Ebr. 12:22*).

## **MLANGO WA SITA: ISAKARI**

**Mwanzo 30:18:** Isakari maana yake ni *Ujira, au Zawadi*. Ujira kwa watu wa sifa ni uwepo wa Mungu, kukaliwa na uwepo Wake. Ujira ni kwamba uwepo unaenda nasi; tunaubeba uwepo wake kama makuhani wa Mungu wa kweli (**Hesabu 4:15, Kumbu 31:9, 1 Nyakati 15:2**). **Efeso 1:6** inasema tulichaguliwa katika Kristo "kwa sifa za utukufu wa neema Yake ". "Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu" (**Kol. 1:27**).

## **MLANGO WA SABA: DANI**

Dani maana yake ni **Mwamuizi**, kutawala (**Mwanzo 30:6**). Tunatawala na kutamalaki maishani kwa njia ya Yesu Kristo! (**Rum. 5:17**) tutatawala duniani (**Ufu. 5:10**). Je, wajua tutawahukumu hata malaika! (**1 Kor. 6:3**) Fanyeni akili, Enyi wafalme, enyi waamuzi wa dunia, mwadibiwe (**Zab. 2:10**).

Kwa njia ya Maombi huku kutawala na kuhukumu kunaanza; tunaitisha ufalme (utawala na kutamalaki kwa Mungu) hapa duniani, tunatangaza maombi na kwa kunena Neno lake mapenzi ya Mungu (**Matt. 6:10**, sala ya Bwana).

## **MLANGO WA NANE: GADI**

Gadi maana yake ni "*Jeshi*" (bahati); Lea alisema, "*jeshi linakuja*" na kumuita jina lake Gadi (**Mwanzo 30:11**). Yakobo anasema Gadi "*atashinda mwishowe*" (**Mwanzo 49:19**). Musa alisema, "*Anakaa kama simba mke, hurarua mkono , naam, na utosi wa kichwa*" (**Kumbu 33:20**). Kuna hali kuwa Gadi anashambulia; Musa anasema, "*Gadi akajichagulia sehemu ya kwanza, kwani ndiko lilikowekwa fungu la mtoa sheria*".

Hii inafwatia mlango wa saba, kuamua ama kutawala. Katika mlango wa Gadi tunajifunza kutumia, na kukaa katika hukumu zake kama jeshi tunashambulia eneo la adui, tukirejesha utawala wa Kristo. Tazama **2 Kor. 10:3-6** jinsi ya kutumia katika Agano Jipy.

## **MLANGO WA TISA: ASHERI**

Asheri maana yake ni *heri* au kutosheleka, kubarikiwa! (**Mwanzo 30:13**). Asheri ni mlango wa Baraka ama dhawabu: Yakobo alisema "*chakula chake kitakuwa kinono, naye atatoa tunu za kifalme*" (**Mwanzo 49:20**).

Musa alisema, "*Asheri abarikiwe mionganoni mwa ndukuze; na akubalike mionganoni mwa nduguze, na achovye mguu wake katika mafuta*" (**Kumbu 33:24**). Mafuta maana yake ni upako. Katika mlango wa tisa, watakatifu wamepitia mambo mengi katika mwenendo wao na Mungu. Kuna dhawabu ama ujira, Baraka ya Asheri: upako.

Asheri pia ni hodari na amesimama mahali pa hukumu (**Kumbu 33:25**). Po pote anapo kwenda (makomeo), ana nguvu kama simba, bali pia analeta hukumu za Mungu (shaba).

## **MLANGO WA KUMI: NAFTALI**

Naftali maana yake ni "*kumenyana*"; Raeli alimenyana na kushinda (**Mwanzo 30:8**). Yakobo alimenyana na Mungu na akashinda (**Mwanzo 32:24-32**). Ni nini kilichotokea wakati Yakobo alimenyana na Mungu? Aliushinda utu wa zamani (Yakobo maana yake ni mtu mjanja au mdanganyifu) na alibadilishwa kuwa mtu mpya, akaitwa Israeli (kumaanisha mtu aliye shindana na Mungu, mfalme wa Mungu). Katika mlango wa kumi – Naftali, tunabadilishwa kabisa kutoka kwa utu wa kale hadi kuwa mtu mpya aliyeumbwa katika Kristo, mtu anayeongozwa na Roho (**Rum 8:14, Galatia 5:25**).

Yakobo alisema Naftali, "*ni Ayala aliyefunguliwa; anatoa maneno mazuri*" **Mwa 49:21**. Musa alisema, "*uliyeshiba fadhili, uliyejawa na Baraka ya Bwana, umiliki magharibi na kusini*" (**Kumbu 33:23**).

Naftali ni mlango wa mabadiliko makubwa katika maisha yetu, kutuweka huru kutokana na maisha ya zamani ili tupokee urithi amba Mungu ametuwekea.

## MLANGO WA KUMI NA MOJA: YUSUFU

Yusufu maana yake ni "*Ataongeza*" (*Mwanzo 30:24*), *kuzaa sana*. Hatimaye baada ya mambo mengi, njia nyingi, vikwazo vingi na mabadiliko, Mungu anatuleta kwa mlango wa kumi na moja ambapo matunda mengi yanazaliwa. *Yohana 15:16*: "*niliwachagua ili mwende mkazaem matunda mengi*". Tumeitwa na kuchaguliwa na Bwana tuzae matunda mengi. Watu amba wamemenyana na Mungu na kushinda, watazaa sana wakiongozwa na Roho na kumtii Kristo, ambaye matunda ni Yake.

*Mwanzo 49:22*: "*Yusufu ni mti mchanga wenyenye kuzaa sana, Mti mchanga wenyenye kuzaa karibu na chemchemi [Chemchemi ya wokovu, Isaya 12:3]; matawi yake yametanda ukutani.*" Yesu ni Mzabibu; nasi ni matawi ya kuzaa matunda (*Yohana 15:5*).

Maneno ya Musa juu ya Yusufu pia yananguvu na Baraka nyingi na ahadi za kuzaa sana: maelfu na makumi ya maelfu! (*Kumbu 33:13-17*)

Ni wakati wa kuzaa sana sasa katika kanisa la Yesu Kristo. Yusufu ni mlango wa Kumi na moja: tuko mwishoni mwa kizazi hiki; ni wakati wa mazao mengi mwisho wa nyakati. Tarajia nyakati za matunda mengi Bwana anavyowatuma watenda kazi katika mavuno.

## MLANGO WA KUMI NA MBILI: BENYAMINI

*Mwanzo 35:18* Benyamini alikuwa mwana wa mwisho wa Yakobo na alizaliwa kwa mke wake aliyempenda sana Raeli aliyega katika kumzaa. Alimwita Benomi, kumaanisha "*mwana wa huzuni wangu*", lakini Yakobo akampa jina lingine kumaanisha, "*Mwana wa mkono wa kuume*". Benyamini ni mlango wa mwisho wa kuingia katika mji Mtakatifu. Kuwa katika mkono wa kuume wa Mungu pamoja na Yesu ndilo lengo letu kuu. Hilo ni lengo la juu ambalo tunaweza kufikia. Yesu aliahidi kanisa la Laodekia hii Baraka katika *Ufu. 3:21*, hakika kuketi pamoja Naye katika Kiti Chake cha Enzi.

Benyamini ni mwenye kuraua-rarua mawindo yake na atabarikiwa na Nyara (*Mwanzo 49:27*). Katika *Isaya 53:12*, Yesu anagawanya nyara na wao walio hodari kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa. Je tunanaja kwa ajili ya nyara? Je, tutaamka na kumtumikia Bwana kama washindi? Musa anamwita Benyamini, mpenzi wa Bwana, atakaa salama Kwake; kwa maneno mengine katika mkono wa Kuume. *Kumbu 33:12*: naye hukaa kati ya mabega Yake ambapo ni mahali pa utawala kulingana na *Isaya 9:6*.

## MLANGO KUMI NA MBILI YA KUINGIA KATIKA MJI MTAKATIFU KWA MUHTASARI:

1. Reuben, Tazama Mwana - Okoka;
2. Simioni, kusikia – Pokea Roho Mtakatifu;
3. Lewi, kuijunga na mwili wa Kristo kuhudumu;
4. Yuda, kufanyika watu wa sifa;
5. Zabuloni, makao, Mungu anakaa katika sifa ;
6. Isakari, ujira, uwepo Wake ni dhawabu yetu;
7. Dani, kuamua ama kutawala, tunaanza kutawala na Kristo;
8. Gadi, Jeshi, tunashambulia (tunashinda);
9. Asheri, heri, kubarikiwa, tunatiwa mafuta ya kuendelea;

10. Naftali, kumenyana, kukabiliana na utu wa zamani, kubadilishwa, kuenenda kwa Roho;
11. Yusufu, ataongeza, kuzaa sana, ni wakati wa mavuno;
12. Benyamini, Mwana wa mkono Wangu wa kuume; tuliingia katika Mji Mtakatifu kwa kukutana na Yesu; hatimaye tunaketi na Yesu katika Kiti cha Enzi cha Baba Yake.

## TAMATI

**Kumbu 33:26:** “*Hakuna aliyefanana na Mungu, Ee Yeshruni,(Israeli) Ajaye amepanda juu ya mbingu ili akusaidie, na juu ya mawingu katika utukufu wake.*”

Mungu atatupatia neema ya kutosha na uweza wa Roho tunaohitaji ili tushinde na kuketi kwenye kiti chake cha Enzi.

**Aya ya 27:** “*Mungu wa milele ndiye makazi yako, na mikono ya milele i chini yako. Na mbele yako amemsukumia mbali adui; akasema angamiza!*”

Anatulinda, kutuweka salama mikononi mwake, anamfukuzia mbali adui wetu.

**Aya ya 28:** “*Na Israeli anakaa salama, chemchemi ya Yakobo pekee yake, katika nchi ya ngano na divai, [mkate, Neno] Divai mpya [Furaha ya Roho]; Naam, mbingu zake zadondoza umande [maji maenge]. Mwanzo 2:6.*

Mungu anatalisha na Neno Lake, Roho wake anatupatia furaha ndani yetu, na maji maenge kila siku.

**Aya ya 29:** “*U heri Israeli. Ni nani aliye kama wewe, taifa lililookolewa na BWANA! Ndiye ngao na msaada wako, na upanga wa utukufu wako; na adui zako watajitiisha chini yako, nawe utapakanyaga mahali pao pa juu.*”

## ISAYA 12

- 1     “Na katika siku hiyo utasema: “Ee BWANA, nitakushukuru wewe; kwa kuwa ijapokuwa ulinikasirikia, hasira yako imegeukia mbali, nawe unanifariji moyo.
- 2     Tazama, Mungu ndiye wokovu wangu; nitatumaniini wala sitaogopa; maana BWANA YEHOVA ni nguvu zangu na wimbo wangu; naye amekuwa wokovu wangu.””
- 3     Basi, kwa furaha mtateka maji katika visima nya wokovu.
- 4     Na katika siku hiyo mtasema, Mshukuruni BWANA, liitieni jina lake; Yatangazeni matendo yake kati ya mataifa. Litajeni jina lake kuwa limetukuka.
- 5     Mwimbieni BWANA; kwa kuwa ametenda makuu; Na yajulikane haya katika dunia yote.
- 6     Paza sauti, piga kelele, mwenyeji wa Sayuni; Maana Mtakatifu wa Israeli ni mkuu kati yako!”